# *UMOJA*

Asante, Ndugu Orman. Bwana akubariki.

Habari za asubuhi, marafiki. Ni vizuri kuwa hapa maskanini tena asubuhi ya leo. Nami nilikuwa tu nimesimama pale nyuma nikisikiliza, nilipokuwa nikiingia, na kuusikiliza unabii ukitolewa katika njia ya kunena kwa lugha, pamoja na tafsiri. Nami nikawaambia hao jamaa kwamba chumba hicho kimejaa pia, kwa hiyo nikasema, "Sijui, sijazungumza na mtu huyu" (Huyo alikuwa ni Ndugu Higginbotham, kama nilimwelewa mtu huyo vizuri.) "kwa muda mrefu. Imekuwa ni miezi tangu hata nimemsalimia kwa mkono." Lakini hilo ndilo hasa ninalozungumzia, yale aliyosema asubuhi ya leo, yale hasa ninayozungumzia. Yeye hakujua hilo. Sikulijua mweyewe mpaka muda mfupi tu uliopita, yale niliyokuwa ninaenda kuzungumzia. Na jambo ndilo hilo tu, yale aliyosema papo hapo. Kwa hiyo tuna furaha kujua ya kwamba tumekusanyika katika Jina la Bwana Yesu, na chini ya mabaya Yake yanayotulinda.

2 Sasa, naona wengi wamesimama, mahali hapa pamejaa na kusongamana, nasi tunachukia tu kuona hili. Na, mara tuwezapo, tutaibadilisha hapa, maskani kubwa zaidi. Sasa, ninataka kutoa taarifa kutoka Phoenix upesi tu.

3 Nilikuwa hapa Jumapili iliyopita usiku na kuzungumza juu ya somo la *Ushirika* kwa . . . kabla ya ibada ya ushirika. Ushirika sio kula mkate, *kushiriki* maana yake "kuzungumza na, kujibu, kuzungumza na mtu fulani."

4 Na sasa asubuhi ya leo, kama nikichukua muda mrefu kupita kiasi kidogo, mbona, mtu abadilishane viti na hao wanaosimama, nalo litathaminiwa, waache waketi chini kidogo. Ni—ninahusika na wakati huu tunaoishi. Ninahusika sana, sana. Ninapoyaona mambo yakitukia ninayoyaona yakitukia, kuna kitu fulani ndani yangu kinachochochewa. Nami ninataka tu kuuchukua wakati wangu na kujaribu kuninii . . .

5 Ujumbe wa asubuhi hii ninazungumza juu ya somo la *Umoja*. Na ni—ninataka kuuchukua wakati wangu na kujaribu kulifanya tu . . . kuliweka kikamilifu tu nijuavyo mimi. Nami ninayatamani maombi yenu mlivyokusanyika.

6 Na sasa ninawatakeni kufungua, endapo unayo Biblia na ungetaka kusoma pamoja nami, kwenye mlango wa kwanza wa Waebrania, kwanza. Nami ninataka kusoma vifungu vya kwanza vitatu vya mlango wa kwanza wa Waebrania, na kisha Mwanzo 1:26 na 7, kuyafunganisha hayo pamoja. Na hakuna mtu anayeweza kusema chochote kinachostahili kusemwa isipokuwa Mungu amsaidie kulisema. Na—na hilo linaambatana na Ujumbe

asubuhi ya leo, pia, wa umoja wa watu na Mungu. Sasa katika Webrania mlango wa kwanza, tunasoma hivi.

> *Mungu ambaye alisema* zamani *na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi . . . kwa njia mbalimbali,*
>
> *Mwisho wa siku* hizi *amesema na sisi* kupitia *wake . . . Mwana wake, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.*
>
> *Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akavichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa ukuu huko juu;*

7 Na sasa katika Mwanzo, m—mlango wa kwanza na kifungu cha 27, 26 na 27, ninasoma hili.

> *Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu: wakatawale samaki wa baharini na* ndege *wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.*
>
> *Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba; mwanamume na mwanamke aliwaumba.*

8 Sasa na tuviinamishe vichwa vyetu kidogo tu tunapoomba. Nami nina hakika kuna haja nyingi katika kusanyiko la ukubwa huu, kwa hiyo labda tumwinulie tu Mungu mikono yetu, yeye aliye na haja, naye kwa hili afanye ijulikane ya kwamba tuna kitu tunachotaka kiombewe. Mungu na amjalie kila mmoja wenu.

9 Bwana, tumekusanyika chini ya paa la maskani hii, nasi tunashukuru kuwa na paa juu yetu leo hii, bali kukutanika kwetu kulikuwa kwa ajili ya kusudi kubwa kuliko hili. Tunajisikia kwamba kwa ahadi ya Mungu tumekusanyika chini ya mabawa ya Mwenyezi. Kwamba Yeye, kama vile kuku angewafunika vifaranga vyake, angetulinda na yote tunayotaka Yeye atulinde nayo. Ya kwamba angetuzungukazunguka na kutulisha na angetupa leo chakula chetu cha kila siku, cha kimwili na cha kiroho pia, tupate nguvu za kuisaidia miili yetu kutembea juu ya dunia, na nguvu za kustawisha za Roho Mtakatifu kulileta Neno la Mungu kwa watu walio na njaa. Kisha kuondoka hapa na Hizo juu ya midomo yetu na mioyoni mwetu, pamoja na Mafuta mapya ya kupaka hata tungeweza kuwaambia wengine juu ya siku tunayoishi, na hali ya wakati. Mungu, tunakutumaini Wewe kabisa. Hakuna mahali pengine palipobaki ambapo hapana mtu angeweza kwenda. Tunajiskia kama Petro alivyojisikia, siku ile wakati Yesu aliposema, "Mtaenda pia?"

10 Yeye akasema, "Bwana, twende wapi? Wewe pekee ndiye uliye na Maneno ya Uzima wa Milele." Na hiyo ndiyo sababu

tumekusanyika katika Jina Lako asubuhi ya leo, kwa sababu Wewe pekee unayo Maneno ya Uzima wa Milele. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utalifanya hili kuwa halisi sana kwa kila mmoja wetu leo hii hata mioyo yetu itawaka ndani yetu. Nafsi zetu zitatiwa nguvu, miili yetu itaponywa, roho zetu zitaponywa, nafsi zetu zitafanywa upya, ziumbwe kama vile Mungu angetutaka.

11 Baba, ninaomba ya kwamba utawapa nguvu wale wanaosimama vyumbani na kuzunguka kuta, na huku kwenye ukumbi. Ninaomba ya kwamba Wewe utawapa nguvu. Na, nikijua hili linaingia kwenye kanda, ambazo zitaenda katika mataifa mengi mbalimbali, katika nchi mbalimbali na makabila ya duniani. Na, Mungu, tunakutumainia Wewe kikamilifu. Tupe tu nguvu na—na Neno na upako, ipate kuwa tu jinsi Wewe ungetaka iwe kwa ajili ya saa hii. Tunajikabidhi Kwako sasa, kusikiliza kwetu, sauti yetu, usikivu wetu, yote tuliyo, tunayakabidhi Kwako, kwamba Wewe ungetenda kazi ndani yetu. Fanya kazi kupitia sisi na uudhihirishe Uwepo Wako mkuu pamoja nasi. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu, Mwana Wako. Amina.

12 Neno *umoja* linamaanisha, “kuwa mmoja na.” *Umoja*, “kuungana.” Na, sasa, hili ni somo kwelikweli, nalo lina—linastahili kuzingatiwa sana kuliko vile ninavyoweza kulizingatia, na kuliko vile karibu watu wote duniani wangeweza kulizingatia. Lakini ningetaka kuwaelezea maoni yangu juu yake, na, pamoja na yale Mungu atakayotupa. Sasa, katika hili, ni kufundisha fundisho. Na kwa ndugu ambao huenda wataisikia kanda hii, natumaini kwamba haitakuwa ni chukizo, bali itakuwa ni kuwafanya mlichukue hili kwa uzito sana, kwa uzingativu, hasa. Kwamba mtalisoma kwa njia ya maombi, kwa uangalifu, na kulipima kwenye mizani ya Neno la Mungu, muone kama Hilo ni la Mungu au la.

13 Kwa kuwa ninaamini kwamba hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya sikuzote, kupima mambo kwa Neno, kwa sababu Neno ndilo Kitu pekee kitakachoweza kusalia. Yesu alisema, “Mbingu na nchi zote zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Hiyo ndiyo sababu ninaliamini Hilo, na kuliamini Hilo kwamba ni mpango wa Mungu. Ninaamini kwamba Hiyo ndiyo kazi iliyomalizika ya Mungu iliyoandikwa katika Neno. Kwa hiyo, kwamba kama chochote kingekuwa kinyume na Neno hilo, kisingeweza kuwa ni Mungu wala mpango wa Mungu. Ninaamini Hilo ni mpango. Sasa, Roho wa Mungu katika Neno hulifanya Neno lijiishi Lenyewe, lijitekeleze Lenyewe. Analifanya Neno kuwa hai, kama vile mbegu.

14 Sasa, mwanamume wa kwanza na mwanamke wa kwanza katika bustani ya Edeni walikuwa katika upatanifu mkamilifu na Mungu, sana hata Mungu angeweza kushuka wakati wowote aliopenda Yeye na kuzungumza mdomo kwa sikio na Adamu na

Hawa. Sasa, huo ni umoja mkamilifu, Mungu na kiumbe Chake, Mungu akizungumza mdomo kwa sikio na Adamu na Hawa. Nao walikuwa katika upatanifu mkamilifu sana na Mungu hata walikuwa mmoja na Mungu. Mungu na familia Yake walikuwa ni mmoja.

15 Mtu yeyote na familia yake, familia sahihi, nzuri, adilifu, tiifu ni mmoja na mwingine, familia yoyote. Na kama kuna jambo fulani katika familia ambalo linawatenganisha, basi si sahihi, familia hiyo imevunjika mahali fulani. Wote wanapaswa kuwa mmoja, baba na mama, mama na baba, watoto na wazazi, wazazi na watoto, wote katika maafikiano. Basi, unapoona hilo, utaona picha moja nzuri.

16 Hilo ndilo kusudi la Mungu. Na kusudi lake kama Baba, mkuu, lilikuwa ni kuwa mmoja na familia Yake, familia ya duniani, Adamu na Hawa. Na njia pekee wangaliweza kuwa mmoja na familia, ama na Mungu, ni kwa sababu tabia ya Mungu ilikuwa ndani yao. Kwa hiyo hiyo iliwafanya kuwa na tabia ya Mungu ndani yao, halafu mmoja kwa mwingine pamoja na Mungu, wote wakawa mmoja. Hiyo si ni picha nzuri, Mungu katika familia Yake, Baba juu ya wote, mkuu! Hakuna mauti, hakuna simanzi, hakuna huzuni, hakuna chochote; furaha tu isiyosemeka; wasiwe wagonjwa kamwe, kamwe wasishikwe na huzuni, mmoja tu pamoja na Mungu! Ni picha ya jinsi gani! Kwa sababu, tabia yenyewe ya Mungu ilikuwa ndani ya watu hawa. Na kwa hiyo, yale waliyofanya, waliambatana tu moja kwa moja na Mungu, na Mungu pamoja nao akawafanya mmoja.

17 Sasa, Yesu aliomba, katika Yohana, mlango wa 17 na kifungu cha 11, kwenu mnaoandika vifungu hivi vya shule ya Jumapili. Ninavyo vingi asubuhi ya leo. Yohana 17:11, Yesu aliomba ya kwamba Kanisa na Yeye wangekuwa mmoja kama vile Yeye na Baba walivyokuwa Mmoja. Kwamba Kanisa, sisi kama washiriki wa Mwili wa Kristo, tungekuwa mmoja, pamoja, kama tu vile Yeye na Baba walivyo Mmoja. Na kwenye siku hiyo tungejua ya kwamba Yeye alikuwa ndani ya Baba. . .Baba ndani Yake, na Yeye ndani yetu, kwamba pamoja tulikuwa ni mmoja. Ni muungano wa jinsi gani, umoja ambao ungekuwa, kumwona Mungu katika Kanisa Lake hata kila mshiriki yuko katika upatanifu mkamilifu kabisa mmoja na mwingine na pamoja na Mungu. Hilo ndilo Kanisa ambalo Yesu analijia. Hapo ndipo maombi Yake yatakapojibiwa, kwamba tutakuwa mmoja.

18 Nao ndio msingi pekee wa ushirika ambao Mungu amewahi kuweka kwa ajili Yake Mwenyewe na Kanisa Lake, ni umoja wa Yeye Mwenyewe ndani ya watu. Huo ndio msingi pekee wa ushirika. Na njia pekee unayoweza kuwa na misingi hiyo ni kwa umoja, kuunganishwa pamoja na Yeye milele. Ni kama tu wakati unapoungana na mumeo, mwanamke kuunganika na mume wake, ni nadhiri idumuyo hata mauti. Sasa, basi unapoungana na Mungu, ni jambo lile lile ambalo kanisa

liliungana na Kristo, ni mpaka mauti yatakapotutenganisha. Halafu basi kama kamwe hutendi dhambi wala kufanya lolote baya, utaunganishwa na Mungu Milele. Nayo mauti tu ndiyo yanayoweza kukuondoa kwa Mungu, na si mauti ya mwili, bali dhambi ya mauti. Dhambi ni mauti, na hiyo hukuondolea mbali na Mungu. Kwa hiyo, kuunganishwa na Yeye katika Roho wa nguvu Zake, ni Uzima wa Milele, umeunganishwa na Mungu Milele. Loo, ninataka kulifikia hilo baada ya muda mfupi. Kuunganishwa Milele na Mungu wa Milele, katika upatanifu mkamilifu na Yeye, kuunganishwa kikamilifu, Kanisa ambalo wote, Mungu na Kanisa Lake pia, ni mmoja, wameunganishwa pamoja.

19 Na kama utaona jinsi Hawa alivyounganishwa na Adamu, yeye alifanyika sehemu yake. Mungu, hivi mliona katika Mwanzo 1:27, Yeye alimuumba mtu mwanamume na mwanamke, Yeye aliwaumba. Sasa, huyo mwanamume alikuwa ninii . . . wote wawili wa kiume na wa kike inapofikia kuwa katika roho ya kike na ya kiume. Ndipo Mungu akatoa kutoka ubavuni mwake u—ubavu. Uliona hiyo sehemu ya mwili ilikuwa ni zaotuka, bali si roho? Sehemu ya mwili wa mwanamke ilikuwa ni zaotuka, baada ya uumbaji kumalizika, Mungu alitoa ubavuni mwa Adamu ubavu na kumfanya mwanamke. Bali si roho, roho ilikuwa ni sehemu ya Adamu, kwa kuwa yeye alikuwa wote wawili mwanamume na mwanamke, kik- . . . tukinena kiroho, wa kiume na wa kike pia.

20 Sasa, hivi hamwoni ile picha kuu? Sisi, katika mwili, ni tofauti. Sisi ni kama zaotuka, kiumbe kilichoumbwa, kwa ndoa takatifu. Lakini katika Roho sisi ni wana na binti, sio roho nyingine, bali Roho wa Mungu aliye hai. Tuko katika sura Yake, katika umoja Wake, katika mfano mkamilifu wa Mungu aliye hai, kwa sababu tunakuwa wana na binti. Sio waliotenganishwa, bali Roho yule yule, Mungu yule yule, Mtu yule yule, waliounganishwa katika ndoa na yule wa Milele. Mnaona jinsi Mungu alivyopanga kwamba tusiwe tofauti, bali Yeye! Si kiumbe kingine cha kabila lingine, bali mwungano halisi na uzao wa Mwenyezi, uliofanyizwa kwa ndoa takatifu. Sasa, mwili hutoka kwa mama na baba, bali Roho hutoka kwa Mungu, Mungu akijigawa Mwenyewe kama vile Adamu alivyogawanywa.

21 Kwenye Siku ya Pentekoste, tunaona Roho Mtakatifu, ile Nguzo ya Moto, ikijigawa na kukaa juu ya kila mshiriki wa Kanisa hilo, Mungu akijiunganisha Mwenyewe pamoja! Halafu pamoja na kundi hilo la watu pamoja, inafanya nini? Inaurejesha Mwili wa Bwana Yesu uliounganishwa. Kuja pamoja!

22 Na leo hii katika utengano huu mkubwa tunamoishi, tofauti za kimadhehebu na kadhalika, ni sikitiko jinsi gani, ni fedheha jinsi gani!

23 Kuunganishwa katika ndoa ya Kimbinguni kwa Mungu wa Milele, sehemu Yake, sehemu ya Mungu. Katika mwili nilifanyika Branham kwa sababu ya Baba yangu, Branham. Unafanyika sehemu ya baba na mama yako, lakini katika roho tunaunganishwa na Mungu, ni sehemu ya Mungu. Hiyo ndiyo sababu roho haiwezi kufa. "Yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa milele. Na katika mfano alio nao hapa duniani, na katika sura yake, nitamfufua katika siku za mwisho." Sio utu wa roho, kwa kuwa tutakuwa na mwili kama mwili mtukufu wa Mungu, mwili uliotukuzwa wa Bwana Yesu, tukiinuliwa katika Mfano Huo.

24 Yesu alisema, akienda kwenye kaburi la Lazaro, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Naye kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kabisa hata milele. Aaminiye *katika* Mimi, sio *juu* yangu, bali *katika* Mimi." Kuwa *katika* Yeye, ukiamini! "Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu ndani yenu." Katika Yeye, ukiamini! Loo, jamani! Ninatumaini Roho Mtakatifu atalishusha hilo moja kwa moja kwenu. Sasa, ninyi ndio lile kundi dogo, hiyo ndiyo sababu kote katika juma, nikiomba na kumsihi Mungu, nilichagua somo hili, kuwaonyesha mahali tunaposimama. Kumwamini Yeye. Huwezi kumwamini Yeye mpaka uingie ndani Yake, ama, Yeye aingie ndani yako, ndipo unamwamini Yeye, basi unao Uzima wa Milele. Unaamini *juu* Yake mpaka utakapoupokea Uzima wa Milele, Uzima wa Milele ni Uzima wa Mungu ndani yako, ndipo unaamini *katika* Yeye.

25 "Ninyi ndani Yangu, Mimi ndani yenu. Wapate kuwa mmoja, Baba, kama vile Mimi na Wewe tulivyo Mmoja." Mungu ndani ya Kristo, Kristo ndani ya Kanisa. Mnaona? "Kama tu Sisi tulivyo Mmoja, wao wapate kuwa mmoja." Basi mnawezaje kuwa mmoja? "Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu ndani yenu." Mnaona, kukaa! "Maneno yangu ndani yenu, basi ombeni mtakalo." Kwa kuwa si wewe tena, ni Neno lililo ndani yako, nalo Neno ni Mungu.

26 Sasa, Neno la Mungu ni Upanga. Waebrania, mlango wa 4, inasema hivyo, Waebrania 4:12. Sasa, ni Upanga. Nao upanga ni bwete kabisa iwapo hautumiwi na mkono ama nguvu fulani. Nao ni . . . bali inahitaji mkono kuushika huo Upanga. Na inahitaji mkono unaoushika Upanga huu, ni mkono wa imani.

27 Sasa, mkono huo wa imani, inategemea jinsi ulivyo na nguvu. Mkono huu wa imani huenda ukawa na nguvu kutosha tu kukata shimo dogo kupitia gizani na kusema, "Kwa imani nimeokolewa." Huo ni mkato mkubwa, lakini, basi, kama hizo ndizo nguvu pekee ulizo nazo mkono huo za kuutumia Upanga huo, hilo tu ndilo unaloweza kukata. Lakini, ikiwa ni mkono wenye nguvu, utakata kupitia kila kitu ibilisi anachoweza kuweka kule, ufanye kila ahadi ya Mungu iangaze katika nguvu za kufufuka Kwake. Kama ni mkono wenye nguvu wa imani, "Siku za miujiza! Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata

milele," kuikata njia yake na kupenya. Inategemea nguvu za mkono nyuma ya huo Upanga.

28 Nao huo Upanga una ukali mwingi. Waebrania 4, kasema, "Ni kali kuliko upanga ukatao kuwili ambao hukata kuja na kwenda pia, na hata unaenda kwenye ma—mafuta ya mfupa, na katika viungo, na huyatambua mawazo ya moyo." Linaenda kupita mambo ya kimwili, linaingia kwenye milki ya kiroho na kuyachukua mawazo ya moyo na kuyafunua. Roho wa Mungu, Neno la Mungu.

29 Sasa, Neno hilo litakata hapo iwapo kuna mkono wa kutosha nyuma Yake kulisukuma ndani, litapata mahali Pake na kukata na kutoa kila ahadi na kukupa wewe, ikiwa tu una mkono wenye nguvu kutosha nyuma Yake. Ule Upanga, utwae katika mkono—mkono wa imani! Ukamate kwa nguvu sana, ushikilie na kukabiliana na adui. Huyo adui asiyetahiriwa anawezaje kusimama Mbele za Mungu wa Milele? Kwa hiyo, wewe chukua Upanga wa Neno, ndipo kila ahadi ni yako. Utwae kwa mkono wenye nguvu wa imani, songa mbele! Kama unahitaji uponyaji, ukate na kuutoa kwa Neno, "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele." Kama unahitaji wokovu, kila ahadi katika Biblia ni yako. Umekaa kule nyuma na Shetani anajaribu kuuficha, lakini uchukue Upanga huo na usukume kupitia gizani mpaka Nuru ya Mungu iangaze juu ya nafsi yako nawe unayo hiyo ahadi. Yeye atafanya hivyo.

30 Adamu alikuwa sehemu ya, ama, Hawa alikuwa ni sehemu ya Adamu, alikuwa ni nyama ya nyama yake na mfupa wa mfupa wake. Na hivyo ndivyo muungano wa kweli ulivyo. Na hivyo ndivyo muungano wa kweli wa Kanisa ulivyo, Roho wa Roho Wake, Neno la Maneno Yake. Kamwe huondoki kwenye Neno, mwaminio halisi wa kweli hatapatana juu ya Neno lolote. Kumbukeni, lilikuwa ni Neno moja tu ambalo Hawa alipatana kwalo, Neno moja. Lakini mwaminio wa kweli hatapatana juu ya Neno lolote. Ataushika Upanga wa Imani kwa. . .katika imani, hasa, Upanga wa Neno, na kudai kila ahadi ya Kiungu aliyoifanya Mungu. Jambo ndilo hilo.

31 Wao walikuwa ni mifano ya Mungu kwetu, jinsi tunavyopaswa kuwa, hao, wakiwepo sikuzote, pasipo kushindwa. Waliponena, Mungu alijibu. Yeye aliwaangalia, kila siku. Usiku, wakati wangeenda kulala, Yeye aliwaangalia. Mchana, Yeye aliwaongoza, akawalisha, akawapenda, akashiriki nao sikuzote, wakati wote. Walikuwa katika mfano wa Mungu, naye Mungu alikuwa ndani yao. Hilo ndilo linalofanya ushirika. Hilo ndilo linalofanya muungano, ni Mungu ndani ya Kanisa Lake. Huo ndio muungano. Mengi yanaweza kusemwa, tuna mahali pengi pa kwenda. Kuunganika na Yeye, ni Uzima wa Milele. Na njia pekee tunayoweza kuunganika na Yeye ni kuja kwenye kila sehemu ya Neno Lake. Hiyo ni kweli, chukua kila ahadi na uiamini Hiyo.

32 Sasa, Hawa alikuwa ameunganika mpaka alipolivunja Neno moja, ama, alipolishuku Neno moja kama ni kweli. Hilo lilimtenganisha. Kila Neno, "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno!" Kwa hiyo tunaweza kuwa katika Mungu, tumeunganishwa, kwa sababu Adamu na Hawa, kabla ya kule kuanguka, kabla ya kule kutokuliamini Neno, walikuwa ni mfano wa kile tungeweza kuwa katika Yeye. Kuunganika na Yeye, ni Uzima; kutengwa na Yeye, ni mauti. Sasa, kama tukizifuata amri Zake!

33 Tunajua sisi hukosea, bali hupaswi kuangalia hilo. Si makosa yako, kwa sababu daima utakuwa nayo. Lakini, unaona, ni kuifuata miongozo Yake, kufuata yale Yeye aliyosema ufanye. Kujikwaa na kuanguka havina uhusiano wowote na hilo. Mtumishi halisi wa kweli, kama akijikwaa, ataamka tena. Akiyumbayumba, Mungu humvuta moja kwa moja akamrudisha njiani, almuradi yuko kwenye jukumu lake. Lakini kama ametoka nje ya jukumu lake, Mungu hawajibiki kwake. Lakini mradi tu yuko kwenye jukumu lake, Mungu anamwajibikia, akijua ya kwamba yeye ni mwanamume tu ama mwanamke. Yeye anawajibika kwa mtu huyo mradi tu wako kwenye jukumu lao.

34 Sasa, Kanisa sasa limeposwa na Kristo kwa ajili ya arusi. Arusi haijafanywa bado, itakuwa kwenye ile Karamu ya Arusi ya Mwana-kondoo. Kwa hiyo, tunaona ya kwamba Kanisa sasa limeposwa, kama vile mwanamume aliyemposa mkewe. Yeye hufanya nini wakati wameposana? Yeye anamkabidhi tu vitu vya kila namna, akimtumia zawadi, akimfanya kujisikia vizuri. Vema, hivyo ndivyo Kristo anavyolifanyia Kanisa Lake. Yeye anatutumia karama za Roho. Unawezaje kuwa umeposwa basi wakati unapokana karama hizi zipo? Ndizo ishara zenyewe za upendo. Ni ishara ya Mungu kwa Kanisa. Yesu alisema hivyo, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

35 Sasa, weka mambo hayo akilini. Kanisa halina budi kuamini kila Neno, kila ahadi, kila nukta, na kuidai Hiyo kwa ajili yao wenyewe, na kujizoeza ndani Yake. Kama nilikuwa nimemposa msichana, nami nilikuwa kapera, ndipo ningemtumia kitu fulani, pete ya uchumba, naye asingeivaa, basi hiyo inaonyesha yeye haniamini. Ha—ha—hataki kuwa bibi-arusi wangu. Na kama Kristo akilitumia kanisa Lake karama alizoahidi, nao wazikatae na kusema "sivyo zilivyo," hawataki kuwa Bibi-arusi wa Kristo. Wameposwa na mpenzi mwingine, wala si Kristo, Bwana-arusi. Kwa hiyo Kanisa halisi huitimiza ahadi, na kuzitimiza zote, na huzikubali karama ambazo Mungu huwatumia. Vema.

36 Sasa, wanadamu wa kwanza walijiondoa kwenye ushirika kutoka kwa kumwamini Mungu, kwa kutokuliamini Neno Lake na kuusikiliza uongo wa ibilisi. Sasa, hilo ndilo jambo la kwanza lililovunja ushirika wa muungano huu wa ajabu. Sasa angalieni, Adamu na Hawa katika mahali ili kamwe wasiweze kufa, katika

mahali ili wasije wakazeeka, wasiwe wagonjwa, wasiwe na wasiwasi.

37 Unasema, "Hakika laiti ningeweza kuwa hivyo." Hebu mimi . . . nina habari kwa ajili yako, uko katika mahali pale pale. Mungu huweka hilo kwa kila kiumbe duniani, mahali pale pale.

38 Mapatano yalikuwa nini? "Kama mtayatii Maneno Yangu! Kama, Neno Langu, kama mtalitii, mliamini na kulitekeleza!" Lakini mara ya kwanza kabisa ambapo Hawa alikosa kuamini, akaondoa Neno moja kutoka kwa yale aliyosema Mungu, ilivunja ushirika pamoja na muungano huo mkuu. Na dakika ile kanisa linapokosa kuliamini Neno lolote moja la Biblia ya Mungu, na kuliweka Hilo mahali pengine, basi wao huvunja ushirika huo wa ajabu waliopewa, na kutengwa. Mara alipofanya hivyo, mauti yaliingia katika mwili wake upatikanao na mauti. Sio tu mwili wake, bali utu wake wa kiroho. Alivunja ushirika na Mungu, dakika ile alipolitilia shaka. Wala hakuna mtu anayeweza kuamini . . . Hili hapa! Hakuna mwanamume, hakuna mwanamke anayeweza—anayeweza kuamini uongo wa ibilisi mpaka wawe wameitilia shaka Kweli ya Mungu. Hakuna mtu anayeweza kuuamini uongo wa ibilisi mpaka wawe wameitilia shaka Kweli ya Mungu. Kwa hiyo, mnaona, Hawa, Adamu, mahali linapotuweka asubuhi ya leo?

39 Sasa hebu tuwazie kwa makini, kwa sababu kamwe hatutaweza kuwazia tena baada ya haya, baada ya maisha haya ya binadamu kuisha. Kuwaza kwako ni sasa. Huwezi kuchagua baada ya haya, huna budi kuchagua sasa, kwa kuwa hii ndiyo siku ya kuchagua, kufanya chaguo lako. Sasa yeye, Neno moja, sio Amri zote, Neno moja tu, yeye alimshuku Mungu kwa sababu liliwasilishwa kwake kwa njia hiyo, kwamba Neno hilo lilitiliwa shaka. Neno la Mungu haliwezi kupigiwa swali, Yeye alimaanisha tu yale aliyosema. Bali yeye alilipigia Hilo swali kwa sababu lililetwa kwake, "Loo, Mungu hakika hakumaanisha hilo." Lakini Yeye kweli alimaanisha hilo! Mungu humaanisha kila Neno analosema. Wala Hilo halihitaji kufasiriwa apendavyo mtu yeyote, Hilo liko vile tu Yeye alivyolisema.

40 Vema, mnasema, "Unajuaje juu ya Biblia." Ninaamini ya kwamba Mungu wangu ameiongoza Biblia hii, Yeye huliangalia Neno Lake. Yeye alijua ya kwamba wakanamungu na makafiri wangeinuka katika siku za mwisho, kwa hiyo Yeye ameliangalia Hilo. Hivi ndivyo hasa Mungu alivyolimaanisha Hilo. Ni jinsi lilivyo kwetu sasa. Sasa hatuna budi kuliamini Hilo. Neno moja kutoka Kwake, nasi tunapoteza ushirika wetu, tunapotoka na kuingia ma—mautini, utengano wa Milele kutoka kwa Mungu, kama tu vile Adamu na Hawa walivyofanya. Hatuna budi kuuamini Ukweli wa Mungu.

41 Hebu niliseme hilo tena. Usikose kuliamini Neno lolote la Biblia ya Mungu. Lakini usiseme tu, "Naam, ninaamini Hilo."

Sema "lakini"? La, hakuna kitu kuhusu hilo. Wewe liamini, utalikubali. Kama ukiliweka Hilo kando, useme, "Vema, kanisa langu haliliamini Hilo hivyo," basi huamini Hilo ni Neno la Mungu, nawe utaondoka chini ya hukumu ile ile Hawa aliondoka chini yake. Ulijitenga na yule wa Milele wakati ulipokuwa na nafasi ya kuunganishwa Naye. Sasa, kumbuka, Hilo haliwezi kupigiwa swali, kwa sababu Hilo lilikuwa ni Neno moja, ambalo, katika Neno la Mungu.

42 Na, sasa, kama Mungu alikuwa na—na Maneno machache tu pale ambayo watu hawana budi kuyatii, na katika hayo Maneno machache moja la hayo liliwakilishwa vibaya, likasababisha mauti, angalieni Maneno tuliyo nayo siku hizi! Mnaona? Hatuna budi kupokea kila moja la hayo, tuyashikilie na kuingia ndani yao kama ahadi kutoka kwa Mungu. Naye mke wa kweli wa Mungu atafanya hivyo, wa kweli aliyechumbiwa akaposwa. Sasa, natumaini mambo haya madogo yanaingia kwenye kilindi sasa ili tuweze kuyashika.

43 Ni nini kitu cha kwanza kilichomfanya Hawa kutokuliamini Neno la Mungu? Ilikuwa ni kwa sababu Shetani alimwahidi hekima nyingi zaidi, "Utakuwa na hekima." Sasa, unaona, jamii ya binadamu daima inatafuta kitu fulani. Naye Hawa alikuwa akitafuta hekima nyingi zaidi.

44 Sasa hebu tusimame kwa dakika moja tu. Hiyo si ndiyo hali ya ulimwengu leo hii? Wanataka hekima zaidi, tabaka bora zaidi, wenye elimu ya juu zaidi, wanataka kitu ambacho ni tofauti, hekima zaidi. Hiyo ndiyo Hawa aliyotaka. Lakini hebu niseme hili pia, kwamba hakuna hekima inayoweza kupita ya Mungu, hata hivyo iko katika hali nyenyekevu sana hata watu wanaikosa Hiyo.

45 Shetani, kama vile nimesema mara nyingi, yeye hung'aa, bali Injili humeka. Loo, kuna tofauti kubwa kati ya kung'aa na kumeka. Hollywood hung'aa, bali Kanisa humeka kwa nguvu na upendo wa Mungu. Hollywood hung'aa. Tofauti kubwa kati ya kumeka na kung'aa. Hatutaki kung'aa. Tunataka kumeka.

46 Siku hizi, ni vibaya sana kuwazia hili, bali makanisa hujaribu kuegemea kwenye akili zao wenyewe, kama tu vile Hawa alivyofanya hasa. Yeye aliwazia, kwa sababu liliwasilishwa kwake, lilionekana halisi sana. Loo, usikose kupata hili. Lilionekana halisi sana, kitu ambacho kingeweza kuongezwa juu ya yale Mungu aliyosema. Ilionekana kana kwamba angepata kitu fulani ambacho Mungu hakuwa amemwambia ni umbali gani tu angaliweza kwenda. Mungu hakuwa amempa mpaka kama vile alivyoiweka bahari wala haiwezi kupita kwa sababu mwezi huilinda. Yeye aliwazia. . . Alidhani Shetani alikuwa na kitu fulani kwenye mpira, kama tusemavyo, kwamba yeye angali angeweza kuwa katika umoja na Mungu, na hata hivyo awe mwerevu zaidi, angekuwa na

elimu bora zaidi. Lakini Mungu alikuwa amemgawia yale hasa aliyohitaji.

47 Na Yeye ameligawia kanisa kitu kile kile. Huko si kugeuza kwa seminari, ama kuingia ama kugeuza kutoka kwa—kwa shule ya Biblia. Bali ni yale hasa yaliyoandikwa, na BWANA ASEMA HIVI! Huwezi kulibadilisha Hilo! Lakini makanisa yanaegemea kwenye ufahamu wao wenyewe. Wa—wanafikiri labda ni ninii. . . kuna kitu fulani walichopangiwa, na ni cha udanganyifu.

48 Inanibidi tu kungoja hapa kwa dakika moja. Ulimwengu wote umewekwa msingi juu ya hilo. Uchumi wote wa taifa hili umewekwa msingi juu ya dhana ya uongo. Nitawaambieni utani mdogo juu yangu mwenyewe, sio utani; bali mnajua sisi sote tunawapenda wake zetu, ama, tunapaswa kuwapenda. Basi nilikuwa nikiangalia kipindi hapa siku moja huko Magharibi, imekuwa ni muda mrefu uliopita, yapata miaka mitatu. Na chumbani mwangu asubuhi moja niliamka, na kulikuwako na televisheni imewekwa chumbani. Nami nikawaza, "Inaonekana kana kwamba ni hali mbaya ya anga." Nikawaza, "Vema, saa mbili wanapaswa kuwa na habari." Ndipo nikachukua kitabu kidogo cha mwongozo, kilisema habari kwenye wakati fulani.

49 Nikafungulia habari, na wakati nilipokuwa nikisikiliza habari, basi niliona ya kwamba katikati ya matangazo ya habari walikatiza ili kutangaza namna fulani ya bidhaa, sabuni fulani ya unga. Nayo yakasema, "Haikubidi kuosha vyombo vyako tena, mama. Jambo pekee unalofanya ni kuviingiza mumo humo majini na kuviacha vitulie kwa dakika chache, uvitwae na kuviweka kwenye kichanja cha kukaushia, yote yamekwisha."

50 Nikawazia, "Nitakuwa shujaa nitakapofika nyumbani." Nikaandika jina lake, bidhaa fulani hii. Nikasema, "Nitamwambia mke wangu, 'Angalia ninayoweza kufanya!'"

51 Kwa hiyo nikaenda nikanunua chupa ya bidha hii *fulani-fulani*, na nikainyunyizia kote majini. Nikamwambia aendelee kuifagia nyumba, mimi ningemwoshea vyombo. Kwa hiyo nikachukua sahani za watoto na kuyatoa makombo, na kadhalika, na mabaki ya mayai, ndipo nikazitia majini na kuziacha zikae kwa dakika chache, kisha nikazitoa na kuziweka pale juu. Kulikuwako na mayai mengi juu yazo kadiri yalivyokuwa wakati nilipozitia mle. Mnaona, ni—ningalipoteza. . . Mke wangu angekuwa amepoteza matumaini kwangu kufikia wakati huo.

52 Mnaona, kwa nini taifa hili, kwa nini hawa. . . taifa hili linaruhusu watu wadanganywe? Hilo halipaswi kukubaliwa kusemwa namna hiyo. Hilo linapaswa kuwa ni kukiuka sheria. Kuhusu matangazo ya kisasa ya sigara, ni fedheha jinsi gani, "Hakuna kukohoa katika gari zima," kila namna yake. Hilo halipaswi kuruhusiwa. Linafanya nini? Linadanganya. Yapo

mauti katika kila moja yao. Kunayo mauti katika kunywa wiski; kubaka, mauaji ya kinyama, wazimu, katika hiyo chupa. Lakini hata hivyo tunakubaliwa kuyaweka kwenye vipindi vyetu na kuyatangaza kama "Ya aina ile babu alikunywa. Furaha zaidi kutoka maishani," namna fulani za vinywaji vya pombe na vileo. Ni kitu gani? Ni udanganyifu. Ni kuweka kitu fulani mbele ya umma wapate kujiua nacho. Na tunaruhusiwa kufanya hivyo.

53 Na hebu niligeuze hilo moja kwa moja. Nayo makanisa kupitia kwa mafundisho ya sharti yaliyobuniwa na mwanadamu, kanuni za imani zilizobuniwa na wanadamu yanaleta ujuvi mkuu mbele za watu, nao wanadanganyika, ambalo ni mauti. Hakuna kanisa litakaloisafisha nafsi yako. Hakuna kanuni ya imani inayoweza kuisafisha nafsi yako. Ni Damu ya Yesu Kristo pekee inayoweza kuisafisha nafsi yako, tiba ya Mungu, Hiyo inaungwa mkono. Kwa hiyo ni uongo tu, bali watu wanaegemea kwenye ufahamu wa wenye hekima, nao unawaua. Na watu siku hizi wanaegemea kwenye ufahamu wa—wa kanuni za imani na madhehebu, na mamilioni kama nguruwe waliochinjwa wanatumbukia kwenye shimo lisilo na mwisho la kuzimu. Ni aibu jinsi gani. Tumekatazwa kuegemea kwenye ufahamu wetu wenyewe. Hatuwezi kujaribu.

54 Mnasema, "Hivi baraza la watu halipaswi kusema zaidi juu Yake kuliko mtu mmoja?" Si kama mtu huyo mmoja anasema Neno la Mungu. Kulikuwako na manabii mia nne wakati mmoja waliokuja mbele ya wafalme wawili, nao wakategemea ufahamu wao wenyewe. Lakini kulikuwa na mmoja aliyedumu na Neno la Mungu na ikathibitika yeye alikuwa sahihi, Mikaya. Inategemea kama ni Neno la Mungu. Chochote kinyume na Neno ni makosa, kinasababisha mauti. Hakuna hekima inayoweza kuipita hekima ya Mungu. Yeye ndiye mwerevu wa werevu wote. Yeye ni—Yeye ni Chemchemi. Yeye ndiye chanzo pekee cha hekima. Kila neno la mwanadamu ni ujinga na uongo, ila la Mungu, kama ni kinyume na la Mungu. Sasa, kama mtu huyo anasema Neno la Mungu, basi si—sio neno la mtu huyo tena, ni Neno la Mungu. Mnaona, si ufahamu wa huyo mtu.

55 Shetani atakufanyia kila namna ya ahadi, lakini hana kitu cha kukupa, kwa sababu yeye hana chochote. Hana wokovu. Shetani ni nini? Chochote kinyume na Neno. Yeye hana wokovu, yeye hana Nuru. Ufalme wake ni giza, mwisho wake ni mauti. Giza na mauti ni ufalme wa Shetani. "Ndugu Branham, rudia hilo tena. Ufalme wa Shetani ni nini?" Chochote kinyume na Neno la Mungu.

56 Sasa, hilo linakata, bali ni wakati wa kukata. Mnaona? Tawi, mti, kama litazaa, halina budi kupogolewa. Wakati umewadia.

57 Chochote kilicho kinyume na kanuni za Mungu, Neno la Mungu, sio Mungu. Ni kitu gani, dhambi ni nini? Haki iliyopotoshwa. Mauti ni nini? Uzima uliopotoshwa. Ufalme wa Shetani ni nini? Chochote kinachoweka kitu fulani kupachukua

mahali pa Neno, chochote, fundisho lolote. Neno moja, neno moja tu. Huenda ukaamini kila chembe, Hawa aliamini kila chembe Yake hadi kufikia lile Neno moja. Neno hilo moja ndilo yote aliyopaswa kutokuamini. Neno hilo moja ndilo yote unalohitaji kutosadiki.

58 Sasa hebu tuliangalie. Njia pekee ya kukaa katika ushirika wa Kiungu, ilikuwa ni kulidumisha hilo Neno. Mungu alisema, "Utafanya *hili*. Usifanye *hili*. Utafanya *hili*, na unaweza kufanya *hili* na kufanya *hili*. Ila usifanye *hili*." Sasa, kipande kimoja tu cha amri ambacho hakutii, nacho kikaanzisha hili jambo lote. Kwa sababu yeye alifanya hivyo, akasababisha kila mtoto mwenye njaa aliyepata kuweko ulimwenguni, kila uchungu wa mauti, kila simanzi, kila huzuni kubwa. Alifanya hivyo papo hapo. Ni jambo la kuchukiza jinsi gani, kutokuliamini Neno la Mungu. Kila mtu anayeugua katika uchungu wa kila mauti yaliyopata kuwako ama yatakayopata kuwako, alilisababisha papo hapo. Kila mtoto mdogo asiye wa ndoa, alilisababisha papo hapo, kila mtoto aliyezaliwa chini. . .nje ya ndoa. Kila dhambi iliyopata kufanywa, yeye aliisababisha papo hapo kwa kutimiza kila Neno moja kwa moja ila mahali pamoja padogo hapa. Yeye—yeye alitoa hoja. Alininii tu. . .Hakulipuuza. Alilifahamu, bali alininii tu. . .Alishawishiwa kufanya jambo bora zaidi kwa kuwa aliahidiwa tabaka bora zaidi la watu, hekima bora zaidi, kujua zaidi juu ya jambo Hilo kama angefanya jambo *hili*. "Wahudumu wetu wana elimu bora zaidi. Tuna tabaka bora zaidi."

59 Hakuna tabaka bora zaidi ya watu ulimwenguni kuliko wale wanaolishika Neno la Mungu. Hao ndio walio bora kuliko wote. Hilo ndilo tabaka la pekee ambalo Mungu huliangalia. Muda kidogo tu na huenda ikawa Mungu atatujalia kuliingilia.

60 Ufalme wake hauwezi kuahidi chochote ila mauti. Hayo ndiyo yote aliyo nayo. Yeye ndiye mwanzilishi wa mauti. Anaweza kuahidi uongo kwa sababu yeye ndiye baba wa uongo. Hawezi kukupa Uzima. Hawezi kukupa Mbingu, yeye hana Mbingu za kukupa.

61 Wazia jambo hilo! Neno moja, kutokumwamini Mungu kupitia ahadi ya ibilisi ama mbinu zake, Neno moja, kunakupeleka katika mateso. Hivyo ndivyo ilivyoanza. Na ikiwa Mungu, katika rehema Zake jinsi Yeye alivyo, angetuma fungu hili la kuzimu juu ya nchi, na kusababisha watoto wadogo wenye njaa, kila namna ya mateso, na kuwaua watu kwa njaa, na mauti duniani, kwa sababu Neno moja, hapo mwanzo, hivi Yeye asingeweza kuliachilia na kuachana na kuwa na wingi wote huu wa mateso? Yeye si angefanya hivyo? Basi kama Yeye hakuruhusia Neno moja pale, akijua ya kwamba haya yangekuwa ndiyo matokeo yake, ni zaidi sana vipi Yeye hataruhusia Neno moja pale wakati mtu atakuwa ndiye

anayeteseka peke yake, yule asiyeamini. Liwazie, ni jambo kuu sana.

62 Sasa, wakati Adamu na Hawa waliposikiliza uongo wa ibilisi, ule mfano mtakatifu wa Mungu uliwaacha, ushirika wao na Mungu ukavunjika. Ushirika wao wa umoja na Mungu ukavunjika. Mara walipousikiliza uongo wa ibilisi, hilo lilivunja ushirika wao. Na dakika ile ile unaposikiliza uongo wa ibilisi, itavunja ushirika wako. Hiyo ni dakika ile ile unapotoka katika Uwepo wa Mungu, kama alivyofanya, ni wakati uliposhindwa kulichukua Neno la Mungu jinsi tu lilivyo.

63 Sasa angalieni, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Sote tunajua kuna Mungu. Na kama Mungu ni sahihi sana kwa Neno Lake, na amedhamiria sana kwamba Yeye atawahukumu watu kwa Neno Lake, basi hana budi kulihifadhi Neno mahali fulani kuwahukumu watu kwalo. Biblia hii Ndiyo. Msisahau jambo hilo. Biblia ndiyo Mungu atakayowahukumu watu kwayo, kwa kuwa Hiyo ilisema katika Ufunuo 22, "Yeye atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake au kuongeza neno moja Kwake."

64 Mnaona, sio tu kusema, "Vema, na—naenda kanisani. Ninaamini. Ni—ni—ninamwamini Mungu." Mbona, kila ibilisi katika hiyo kuzimu anamwamini. Kila mmoja wao ni wa kidini, kila mmoja.

65 Lakini inahitaji tu neno moja, hilo linavunja ushirika papo hapo. Mnyororo hauna nguvu zaidi kuliko kiungo chake kilicho dhaifu sana. Na ambapo udhaifu wako ulipo katika kutokuliamini Neno la Mungu, hapo ndipo unapotaka kuweka kiungo kipya, chenye nguvu pamoja na hivyo vingine. Iwapo unaamini Yesu Kristo huokoa, basi huna budi kuweka kiungo mle ndani kinachoamini kwamba Yeye huponya. Kama unaamini Yeye alikuwako, huna budi kuamini Yeye yupo. Haleluya! Kama unaamini Yeye alikuwako, na kushangaa kama Yeye yupo, kiungo hicho kitavunjika, ndipo umepotea. Mnaona ninalomaanisha? Ni kali, ni gumu, bali ni Kweli. Huna budi kumwamini Yeye, kila Neno, kila kitu alichosema.

66 Sasa, mnasema, "Vema, sasa, Ndugu Branham, vipi kuhusu madhehebu haya?" Vema, sasa sikilizeni. Kama yapo pamoja na Neno hili, vema. Lakini kama yakilikana Neno hilo, basi si sahihi, ni ibilisi tena. Mnaona?

67 "Vipi kuhusu kanisa *fulani* hili?" Sijui ni nini kuhusu kanisa hilo. Jambo pekee nijualo ni kulihusu Neno hili. Sasa, utaliaminije kanisa wakati kuna madhehebu mbalimbali mia tisa na kitu, na kila moja likisema "dhehebu letu linao Ukweli hasa"?

68 Sasa ungeenda wapi? Huna budi kuwa na imani katika kitu fulani. Vema, unasema, "Ninayo imani katika Methodisti, katika Baptisti, katika Presbiteri, katika Lutheri, katika Pentekoste, katika Katoliki," chochote kilicho. Unayo imani katika dhehebu

hilo, na, ikiwa ni kinyume na hilo Neno, unafanya jambo lile lile alilofanya Hawa. Hakika! Unafanya jambo lile lile hasa alilofanya, kulichukua Neno la Mungu na kulifanya Hilo . . .

69 "Vema, kuna tabaka bora la watu wanaoenda hapa. Ni jengo kubwa zaidi. Wao ni watu werevu zaidi." Hilo halina uhusiano wowote nalo. Shetani ni mwerevu zaidi kuliko Hawa. Yeye hakuninii . . . hata hakuwa kwenye picha. Bali hakupaswa kuwa mwerevu, alipaswa kuwa mtiifu. Hatupaswi kuwa werevu. Yesu alisema wana wa ulimwengu huu, ama, ufalme wa ulimwengu huu ni mwerevu zaidi, watoto wa giza kuliko watoto wa Nuru. Tunafananishwa na kondoo. Kondoo hawawezi hata kujiongoza wenyewe, hawana budi kuwa na mchungaji. Mungu hatutaki tuwe werevu, Yeye anatutaka kuzitegemea akili Zake, amina, mahali tu Yeye aongozapo. Amina. Mnaiona hiyo picha? Usizitegemee akili zako mwenyewe. Methali 5, 3. Usizitegemee akili zako mwenyewe, tegemea akili Zake. Haijalishi inaonekana ni kinyume namna gani, na jinsi nuru kubwa zinavyoonekana angavu hapa nje, usizijali. Tegemea tu akili Zake, yale Yeye aliyosema ni Kweli.

70 Sasa, umoja katika ushirika ulivunjwa kati ya Mungu na watoto Wake, mara alipokosa kuamini aya moja ndogo, Neno moja dogo la Mungu. Kila mtu anayepata hilo, aseme, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sio Biblia; wasema, "Siiamini Biblia hata kidogo. Ninaamini nusu Yake." Ilimbidi kuiamini yote, kila sehemu.

71 Si hilo tu, bali umoja kati ya mume na mke ulivunjwa. Siamini kuna ndoa yoyote inayoweza kuwa vile inavyopaswa kuwa pasipo muungano kati ya mume na mke na Mungu. Hiyo ni kweli. Watawazaa watoto ulimwenguni, na kuwafanya haramu, wawape sigara, wiski, kucheza karata mbele zao, wanywe pombe mbele zao. Haijalishi ni waaminifu jinsi gani kwa nadhiri zao za ndoa, huko ni kujuana kimwili, huo ni mwili. Lakini kuna roho mle ndani, roho hiyo ya baba na mama wenye dhambi, haidhuru ni waaminifu jinsi gani kwa watoto wao, watatokea vibaya.

72 Vema, mnasema, "Ninawajua wanaume na wanawake ambao hawakuwafundisha watoto wao hivyo, nao hawakuwa Wakristo." Jambo lenyewe la kutowaongoza kwa Kristo lilikuwa ndilo jambo baya kuliko yote waliloweza kufanya mbali na hilo lingine; kutowaongoza kwa Kristo, mnaona. Kwa hiyo huwezi kuwa na muungano sahihi pasipo hilo. Ushirika ulivunjika.

73 Ndipo mara ushirika ulipovunjwa kati ya Adamu na Hawa . . . Punde tu ushirika wao ulipovunjika kati ya Mungu na wao, basi ushirika wao mmoja kwa mwingine ulivunjika.

74 Sikilizeni! Wakati wowote kanisa linapouvunja ushirika wake, kujitupa lenyewe katika dhehebu, ushirika wa waaminio unavunjika. Hatuna budi kuamini kwa moyo mmoja, nia moja, na uwiano mmoja. Hivyo ndivyo walivyokuwa kabla ule

muungano haujapata kufanyika kwenye Siku ya Pentekoste; moyo mmoja, nia moja, na uwiano mmoja. Basi unapolitupa kanisa katika shirika, utapata kila namna ya migongano ndani yake. Kwa sababu, baadhi ya hao watoto mle ndani watamwamini Mungu, watashikilia jambo lililo sahihi, na hao wangine wataenda njia nyingine. Kwa hiyo, huna ushirika. Naam.

75 Kitu gani? Mawazo yake yalibadilika. Loo, naam, mawazo yake yakabadilika. Ushirika Wake na mume wake haukuwa ni sawa. Walianza kukwepa wajibu. Mnaona? Mawazo yake kweli yalibadilika. Kwa nini? Alikuwa na uhai wa ibilisi ndani yake. Kweli kabisa! Mara alipokosa kuliamini Neno la Mungu, alikubali uhai wa ibilisi kwa kuwa aliyakubali mafundisho yake.

76 Ninaweza kulifanya hili gumu sana papa hapa, bali liko kwenye kanda. Nina hakika mnaelewa, Kanisa.

77 Yeye alikosa kuliamini Neno la Mungu nalo likamwondosha kwa Mungu, kwa sababu ndani yake wakati uo huo mlikuwamo na uhai wa ibilisi. Alikuwa ameamini uongo wake, kasema, "Haya matunda ni mazuri," naye akayala pamoja na mumewe. Hiyo ni kweli.

78 Sitalishikilia Hili, nitaliacha lije haidhuru. Kamwe siwezi. Hivi majuzi huko California, ninamaanisha huko Arizona, nilikuwa nikifundisha katika kanisa moja. Kamwe sijawahi kusema lolote chini ya uvuvio ambalo ilinibidi kughairi. Wengi sana wa wahudumu waliniandama juu ya uzao wa Shetani, uzao wa nyoka. "Yule mwanamke, ilikuwa ni kula tofaa." Huh! Hilo, vema, Kaini alifikiria jambo lile lile, yeye akaleta matunda ya kondeni, mnaona. Haikuwa ni tofaa! Kwani alitambuaje alikuwa uchi? Tumepitia hayo. Kweli ilikuwa ni tendo la kujuana kimwili. Bila shaka, ilikuwa hivyo, yeye alitambua alikuwa uchi. Naye alimzaa mtoto kwa yule nyoka, ambaye hakuwa ni mnyama mtambaaji, yeye alikuwa ni mwerevu sana kuliko wanyama wote. Alikuwa ndicho kitu cha pili baada ya mwanadamu. Mwanadamu anaweza kupata tumbili na masokwe—masokwe, na kadhalika, bali hawawezi kupata kiungo hicho kinachomwunganisha mwanadamu na mnyama pamoja. Huyo hapo. Mungu alimlaania mbali sana asingeweza kurudi tena, hilo ni juu yake kwa tendo hili ovu alilotenda. Yeye alikuwa ndiye mbegu pekee ingaliweza kuchanganyana.

79 Sasa, hivi majuzi, nikisimama, nikihubiri, kulikuwako na kundi la Wakatoliki kwenye kusanyiko langu, nami nikasema, "Enyi Wakatoliki mnaomwita Yesu, ama, mnaomwita Mariamu, hasa, 'mama wa Mungu,' Mungu anawezaje kuwa na mama wakati Yeye ni wa Milele? Hawezi kuwa na mama. Yesu hata hakuwa chochote kwa Mariamu, bali Yeye alikuwa tu ni . . . alikuwa ni kiangulio ambacho kilimwangua Yeye."

80 Vema, sikuzote waliamini, nami mwenyewe nilikuwa na wazo lake miaka kadhaa iliyopita, ya kwamba kule—kule kuchukuliwa mimba pasipo na dhambi ya asili kulikuwa ni kwamba Mungu alimtia uvuli na kuweka seli ya damu mle ndani, bali lile yai lilitoka kwa huyo mwanamke. Ikiwa hilo yai lilitoka kwa huyo mwanamke, hapana budi pawe na mhemko kulishusha hilo yai kupitia kwenye tyubu kuingia tumboni. Unaona vile unavyofanya na Mungu? Unamwingiza katika mchafuko wa kijinsia. Mungu, Yule aliyeumba seli ya damu, aliliumba yai, pia. Daktari, hapana budi pawe na chavua ya kiume na ya kike. Hiyo ni kweli.

81 Vema, basi, kama mwanamke huyu alitoa yai, basi Daudi angewezaje kusema "Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu"? Basi kama hilo yai la mwanamke lilikuwa katika Kristo, basi huyo mtu ana jambo la kufanya na sehemu Yake katika ufufuo, wakati wote ni mkamilifu pamoja na Mungu. Ni kwa nini Mungu akaiweka sehemu ya jinsia ya mtu? Katika ufufuo, kwa nini Yeye hakuuacha mwili Wake uone uharibifu? Kwa sababu Yeye alikuwa ni mtakatifu. Na Yeye angekuwaje mtakatifu kama alikuwa na utungaji mimba na Mariamu, nayo chavua ilikuwa imetoka kwa Mariamu, lile yai likashuka kupitia kwa tyubu likaingia tumboni? Ingebidi kuwe na mhemko fulani kulishusha hilo yai chini. Basi huyo mwanamke angekuwa . . .

82 Vema, mnasema, "Huenda hilo yai lilikuwa limekaa pale. Ingeliwezekana." Lakini hilo, kama ndivyo, basi angalia kinachotukia hapa, basi Yeye kwa jumla hakuwa Mungu. Yeye hakuwa Mungu, kiasi kwamba Yeye alikuwa ni mwanadamu. Lakini basi kama ndivyo ilivyo, huyo mwanamke alikuwa na jambo fulani katika hilo. Nayo mbe—mbegu yenyewe iliyotoka kwa Mariamu, iliyotoka kwa mama yake, na mana yake, na mama yake, ilikuwa na kitu fulani cha kibinadamu kilichochanganywa nayo, pamoja na tamaa ya kibinadamu. Isingewezekana. La, bwana. Nilisema, "Yeye . . . alikuwa tu ni . . ."

83 Ni kama vile tu unavyomchukua tai na kumwacha atage yai, kisha uliweke chini ya kuku, huyo kuku ataliangua hilo yai, yeye ni kiangulio tu. Lakini hakuna chembe moja kulihusu, huyo tai, ambayo ni kuku. La, bwana. Huyo kuku alikuwa . . . Ungeweza kumfunga mtoto mdogo wa mbwa juu ya ya—yai la ndege, nalo lingeangua ndege, hicho kijibwa kingeangua. Ni joto la mwili lililoliangua hilo yai.

84 Na hivyo ndivyo ilivyo na Yesu. Mariamu alikuwa tu ni kiangulio. Mungu alimtumia kama anavyomtumia mwanamke mwingine yeyote. Yeye alikuwa ni bikira, hakuwa amewazaa watoto. Yeye aliingia katika tumbo la uzazi la bikira, bali Mungu Muumba aliumba yai na chembe hai pia, aliiumba. Kwa hiyo, ilikuwa ni kuchukua mimba pasipo dhambi ya asili.

85 Nilipotoka nje, hakika, mnajua hao ndugu walikuwa wakiningojea. Wakasema, "Ndugu Branham, ninataka kukuuliza jambo fulani. Ulifanya kosa. Sasa tumekushika."

Nikasema, "Vema, hivyo ndivyo ninavyotaka, kushikwa."

86 Ndipo kasema, "Ulifanya kosa kwa kusema hivi, ulipohubiri *Uzao Wa Nyoka*. Sasa unasema ya kwamba—ya kwamba lile yai lilikuwa la . . . Mungu aliliumba, hilo yai. Kilichotukia, tunaona hapa kwamba katika Mwanzo mlango wa 3, Mungu alimwambia Mariamu, 'Nitaweka uadui kati ya uzao wako na uzao wa nyoka.'"

87 Nikawazia, "Loo, jamani!" Sijawahi kuhubiri chochote maishani mwangu chini ya uvuvio kilichonibidi kughairi, maana sizitegemei akili zangu mwenyewe. Na ikiwa akili zangu ni kinyume na Neno la Mungu, basi akili zangu zimekosea. Lazima iwe ni Neno la Mungu. Kama silo, achana nalo, si la kweli. Lakini sasa kulirarua Hilo ndilo jambo la kufanya. Moyoni mwangu, nikasema, "Baba wa Mbinguni, unisaidie. Sijui la kufanya hapa. Mtu huyu anayo Maandiko, anayaelekezea kidole, 'Nitaweka uadui kati ya uzao wako na uzao wa nyoka.'"

88 Sasa, hili hapa! Roho Mtakatifu akasongea hapo. Ninaamini yeye Yule ambaye angeweza kumtia Mariamu uvuli, ambaye angeweza kuumba, Yeye anaweza pia kuweka Neno kinywani mwako. Ninamtegemea Yeye kila siku. Na daima ni Neno Lake. Hawezi kusema ninii . . . jambo fulani kinyume na Neno Lake. Ndipo kama ukisema umetiwa mafuta, na kuhubiri dhidi ya Kweli za Mungu, basi si upako wa Roho Mtakatifu. Maana, wakati Roho Mtakatifu anapokutia uvuli, Yeye huleta kitu kile kile, maana Hilo ni Neno.

89 Sikilizeni. Ni jambo gani lililotukia? Nikasema, "Vema, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Mwanamke hana yai. Hana uzao. Yeye alisema sasa, Yeye hakusema 'yai,' alisema 'uzao wako.' Na yeye hakuwa na uzao."

90 Inahitaji muungano kufanyiza uzao. Hiyo ni kweli, daktari? Hapana budi. Kama una lundo zima la nyama ya matunda hapa, hazikuwa na uhai ndani yake, ukazipanda hapa nje, ha—hazingechipuka kamwe, zingekaa hapo na kuoza. Nawe usingeweza kupanda huo uhai bila ya kuwa na nyama ya tunda. Kwa hiyo, mnaona, kitu hicho chote ni muungano. Ninajaribu kuwaambia sasa kuhusu Kristo na Kanisa. Ni muungano. Mnaona, ikiwa mwanamke ni mbegu yake mwenyewe basi yeye hahitaji mwanamume, yeye mwenyewe anaweza kujizalia mtoto. Lakini hawezi, hawezi kuzaa mtoto mpaka awe amekuwa na mume, kwa sababu inachukua wawili pamoja kufanyiza uzao. Hiyo ni kweli? Hebu panda mbegu bila uhai ndani yake, uone litakalotukia.

91 Kama walivyo na msemo huu mwanamke huyu kuwazaa hawa mbwa hapa. Mnaona, wasingekuwa hai. Haingewezekana, maana, mnaona, hiyo chavua haitachanganyikana.

92 Sasa, angalieni hili sasa, hu—huyo mwanamke hakuwa ni uzao. Kwa hiyo, Yeye alisema, "Nitaweka uadui kati ya uzao wako na uzao wa nyoka." Akimwambia ya kwamba, Yeye Mwenyewe, atampa uzao, sio kwa kujuana kimwili, kijinsia. Ataumba ndani yake mbegu. Vema, mnasema, "Huo ungekuwa ni uzao Wake?" Naam. Ungekuwa ni wa Mariamu basi baada ya Yeye kumpa. Hili ni jicho langu, Yeye alinipa mimi hili. Ni jicho langu, bali Yeye alinipa. Huu ni mkono wangu, Yeye alinipa. Hii ni sauti yangu, bali Yeye alinipa mimi. Mnaona? Nao huo uzao uliokuwapo, Mariamu . . . haukuwa na uhusiano na Mariamu. Ulikuwa ni jambo fulani Mungu alilotenda Mwenyewe.

93 Kwa hiyo ule uzao uliokuwa ndani yake basi, ulikuwa ni muungano wa tendo lisilo halali, ambao ulikuwa ni mauti. Alikuwa tayari ametiwa mimba na uzao wa nyoka, maana alikuwa ameishi na . . . Ndipo akageuka na kusema, mwenyewe, "Nyoka alinidanganya." Hiyo ni kweli. Na, mara, Kaini akaja.

94 Loo, tunajua yeye alisema alimpata mtoto kutoka kwa Mungu. Bila shaka, kila mtoto anayezaliwa, wa haramu na chochote kingine, hana budi kuja kutokana na tendo la Mungu. Yeye Ndiye pekee Ambaye anaweza kufanya uhai. Bila shaka. Hiyo ni kweli.

95 Mnaona, tayari alikuwa mja mzito. Nalo hilo kamwe . . . jambo tu lililofanya, ni kuitatua ile hoja ya uzao wa nyoka. "Uzao ulio ndani yako sasa ni kwa kutiwa mimba, tendo lako haramu dhidi ya Neno Langu, pamoja na kitu hiki hapa, nawe sasa una uzao wa nyoka. Bali nitakupa uzao kwa kuzaliwa bila ya dhambi, nao Uzao Wake utakiponda kichwa cha nyoka, nacho kichwa chake kitakiponda kisigino." Amina. Acha tu Mungu alipate, kama ni Neno Lake Yeye atalitimiza.

96 Hiyo ndiyo sababu inakupasa kuwa katika muungano na Mungu. Hiyo ndiyo sababu Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, baada ya Yesu kusema "mkawabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," Petro aligeuka na kusema "mkawabatize katika Jina la Yesu Kristo," kwa sababu Jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni Bwana Yesu Kristo. Mnaona hilo? Inahitaji muungano.

97 Paulo kamwe hakuwa amemwona Petro, bali Roho Mtakatifu yeye yule, katika muungano uo huo (utukufu!), alimfanya kusema jambo lile lile. "Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Alisema, "Hatujui kama kunaye."

Kasema, "Mlibatizwaje?"

Kasema, "Kwa Yohana."

98 Kasema, “Hamna budi kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo.” Nao wakampokea Roho Mtakatifu.

99 Ilikuwa ni kitu gani? Ule muungano, kusema jambo lile lile Mungu asemalo! Na hayo ni maungamo. *Ungama* maana yake ni “sema jambo lile lile.” Na Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, kutekeleza yale Yeye aliyosema. Tunasema Hilo ni Kweli, na Yeye analitekeleza. Loo, jamani! Haya basi. Huko hapo kutiwa mimba.

100 Sasa angalieni jinsi ambavyo yeye—yeye—muungano wake kati yake na mumewe ulivyovunjika. Mnaona, upesi, mara Mungu aliposema “Adamu, ulifanyaje jambo hili?” Badala ya kumtetea mke wake, yeye alimlaumu mke wake. “Mwanamke uliyenipa Wewe.” Muungano ukavunjika. Mnaona?

101 Mke alifanya nini? Badala ya kumpenda mumewe na kusema Kweli, yeye alisema uongo. A—a—a—alipaswa kusema, “Yeye hana hatia, mimi nilimpa.” Amina. Biblia ilisema, “Akampa na mumewe.” Alipaswa kusema, “Mtu huyu hana hatia. Nilimpa naye akala, bali mimi ndimi niliyempa.” Badala yake, akamlaumu nyoka, mkato wa karibu sana.

102 Hilo ni jambo lile lile wanalojaribu kufanya siku hizi. Mnaona, mume, mke, muungano umevunjika. Mume na mke, ushirika ulivunjika kati yao. Ule umoja wao ulivunjika, umoja kati yao na Mungu ukavunjika. Kitu hicho chote kikaharibika. Kwa nini? Kwa sababu Neno moja halikuaminiwa. Loo, ndugu, jamani! Naam, alipaswa kusema Kweli. Umoja kati yake na mumewe ukapotea, na umoja wao na Mungu ukapotea. Na kila kanisa lisilochukua Neno lote la Mungu, jambo lile lile hutukia. Ninalipenda Hilo, nanyi je?

103 Angalia kifungua mimba chake, Kaini, mwuaji, mwongo, mdanganyifu, mwenye wivu, alimwonea ndugu yake wivu. Ndugu yake alizititii Amri za Mungu, naye Mungu alikuwa amefanya upatanisho kwa kumchinja sadaka na kumtoa kwa ajili yao. Angalia ujinga wa hilo sasa, wa Shetani, alijaribu kuweka kibadala fulani. Mungu, Biblia ilisema, aliendа akawafanyia nguo za ngozi; kupata ngozi, ilibidi kitu fulani kife. Adamu alijaribu kujifanyia nguo kutoka kwa majani ya mtini. Isingefanya kazi, uhai wa mimea. Uhai, ilibidi uhai unaotembea ufe. Kwa hiyo Yeye akaua uhai wa kiwango cha chini zaidi, na kusema mle ndani kwamba “Siku moja Uhai Wangu Mwenyewe utatolewa kwa ajili yenu, ule Uhai halisi utakaotolewa katika muungano huu tena.” Sasa, tutalifikia katika dakika chache, Mungu akipenda. “Mnaona, huu hapa uhai wa mwana-kondoo. Sasa, jizungushieni hii na kuuficha uchi wenu.” “Hampaswi kula matofaa”? Upuuzi! Mnaona? “Jizungushieni ngozi hizi.” Ilimbidi aue kitu fulani.

104 Naye mwana wa Shetani, hakuja jinsi Yeye alivyotaka, alikuja. Vyovyote unavyotaka kulisema, lakini ilikuwa ni

mwana wa Shetani, maana usafi huo wa Adamu kwa Mungu usingaliweza kuleta kitu cha namna hiyo. Mwangalieni basi mwana wa Shetani, akijaribu kufanya upatanisho, alirudi na jambo lile lile ambalo karibu watu wote husema siku hizi, kichala cha matofaa na matunda ya nchi, kutoa kwa ajili ya upatanisho, kiuasumu.

105 Naye Habili mwenye haki alifanya nini? Yeye alijua kwamba hakikuwa ni kitu kama kula matofaa. Yeye alikuwa ni damu ya mama yake na baba, uhai wao. Kwa hiyo akaleta mwana-kondoo, kama tu Mungu alivyofanya. Haleluya! Yeye alilitii Neno la Mungu, naye Kaini alimwonea wivu.

106 Jambo lile lile siku hizi! Akaja katika dhabihu hiyo ya damu, Neno hilo la Mungu vile hasa linavyosema, akadumu moja kwa moja na Hilo. Wengi wao wangeamini sadaka hiyo ya damu, hakika, lakini ukisema kitu kingine katika Neno, wanasema, "Loo, la, siamini hilo. Aa-ha, hilo—hilo ni kwa ajili ya siku nyingine." Ibilisi yule yule wa kale, ujanja ule ule wa kale! Ngojeni mpaka tutakapolimaliza. Angalieni, yeye alishuka jinsi ile ile.

107 Lakini Kaini, katika njia zake za kipumbavu, sio za kipumbavu sana, bali katika njia zake za kijanja, alidanganyika, naye akaleta tunda. Adamu aliweka . . . Habili alilitimiza Neno la Mungu, akaleta mwana-kondoo. Mungu alisema, "Hiyo ni kweli, Adamu, umetimiza . . . Ama, Habili, umelitimiza Neno Langu." "Kaini, ulijua haikuwa . . . Ni wapi nilipochukua baadhi ya majani ya mtini kama vile baba yako alivyojaribu kufanya? Una kichala cha mitini ama zabibu ama matofaa ama chochote ulicho nacho hapa. Na sasa baba yako alichuma majani kutoka mtini, kujaribu kufanya upatanisho, na hapa wewe unajaribu kuleta tunda kutoka mtini." Haikuwa ni hayo! Ilikuwa ni damu kutoka kwenye uhai.

108 Loo, Mungu aliishusha, kasema, "Hii hapa." Naye Habili alitoa iliyo sahihi. Ndipo ndugu yake akamwonea wivu. Angalieni kile alichofanya, alimwua ndugu yake. Mungu akamwinua mwingine; kama kifo, kuzikwa, na kufufuka kwa Kristo. Angalieni. Mungu basi, ninii Yake . . . Yeye aliwaambia nini Adamu na Hawa? "Enendeni mkaongezeke na kuijaza nchi." Mkaitawanye jamii ya binadamu kote ulimwenguni, kwa hiyo Yeye angeweza kuwashughulikia kibinafsi mpaka Yeye aweze kuwarudisha pamoja. Kuwashughulikia watu, binafsi, kila mtu. Bali hawakulitaka jinsi hiyo.

109 Usiukose ufunuo huu. Mungu, jalia litukie. Naomba mlione jinsi ninavyoliangalia.

110 Mnaona, haikuwa hivyo, Mungu hashughuliki na mtu katika kikundi. Mungu hawashughulikii ninyi katika dhehebu. Yeye anakushughulikia kama mtu binafsi, mtu binafsi. Kibinafsi sisi tumebatizwa kwa Roho Mtakatifu. Kijumla tunabatizwa katika

ule Mwili tunapobatizwa kwa Roho Mtakatifu. Kibinafsi, kila mmoja hubatizwa kwa Roho Mtakatifu, Mungu akishughulika na kila mmoja. Hilo ndilo lililokuwa kusudi Lake, kuwatawanya kote ulimwenguni kusudi apate kuwashughulikia kibinafsi.

111 Lakini badala ya hilo, ni kitu gani kilichotukia? Ilimbidi Mungu kuwatenganisha watu wa Kaini na wa Sethi. Alimfukuza Kaini. Aliwatenganisha ili aweze kulishughulikia kanisa Lake. Angalieni. Kaini alitengwa. Sasa angalieni. Mungu alimtenganisha Kaini mwovu wa Hawa kutoka kwa Sethi mtakatifu wa Adamu. Loo! Hivi Yeye alifanya hivyo? Kupitia kwa tendo lisilo halali, mwanamke huyu akiishi na mtu mwingine na kuzaa mtoto. Mungu alimtenganisha mtoto huyo na kizazi chake kutoka kwa mtu huyu mwenye haki na mtakatifu, watoto wake.

112 Ni jambo lile lile leo hii, kutenganisha, kutenganishwa, akawakuta, hawakuwa katika umoja. Wasingeweza kuwa na umoja. Usiku unaweza kuwa na umoja na mchana? Mwaminio anaweza kuwa na umoja na kafiri? Mtu anayeliamini Neno lote la Mungu anaweza kuwa na umoja na hao wanaoamini tu sehemu ya Neno la Mungu? Mungu anataka watenganishi.

113 Sasa, Kaini alikuwa mwana wa Hawa, yeye alisema, "Nimempata mwana." Lakini Sethi alikuwa mwana wa Adamu. Ndipo Mungu akawatenganisha kwa sababu asingemwacha . . . Mbona, wangepotoshana, watoto waovu wa Kaini wangewapotosha watoto wazuri wa Sethi. Hiyo ni kweli.

114 Sasa tazameni! Naye ibilisi yule yule wa kale aliyemfanya Hawa kutokuliamini Neno moja la Mungu, na kuwaambia wajitenge wenyewe kwa wenyewe na waishi tofauti, kila mmoja, ibilisi yuyo huyo aliingia miongoni mwao na kuwaleta pamoja tena. Mlilipata hilo? Semeni, "Amina," kama mlilipata. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Aliwaleta pamoja tena chini ya muungano haramu, tendo la Mungu . . . kinyume na mpango wa Mungu. Ni jambo gani lililotukia? Alifanyaje jambo hilo? "Wana wa Mungu," ilisema Biblia, Mwanzo, "waliwaona binti za wanadamu." Wana wa Mungu, watoto wa Sethi, waliwaona binti za wanadamu, watoto wa Kaini, jinsi walivyokuwa warembo. Hum! Basi, walifanya nini, waliwatamani! Nao wakaungana pamoja tena, kwa sababu ya urembo, kwamba "walikuwa ni wazuri kwa kuonekana."

115 Jambo lile lile siku hizi! Haya basi, ndugu zangu. Enyi wanyonge wa Kipentekoste, ambao Mungu aliwatenganisha na kuwatuma huko nje mkafanyike wasio wa kimadhehebu! Hamwezi kuiundia pentekoste dhehebu. Aliwatuma huko nje mpate kuwa watu Wake. Lakini mliyaona yale makanisa makubwa mazuri na theolojia, mkajipatia shule nyingi kubwa na kadhalika. Ndipo mkafanya nini? Mmewaunganisha watu wa Mungu tena pamoja na dhehebu, ambalo, msingi wake hasa ni Ukatoliki. Makanisa mazuri, makubwa, watu waliovalia

nadhifu, meya wa jiji na hao wengine wote huja, waliovalia nadhifu sana, wenye elimu iliyo bora zaidi, wanatheolojia wa juu, wanaojua jinsi ya kufikia mahali ambapo kila mtu anavalia mavazi ya kuvutia macho sana, naye mchungaji anasimama kikamilifu sana mahali pake. Ni kitu gani? Mnaviangalia vitu ambavyo Mungu alihukumu. Nanyi mmelichukua kanisa la Kipentekoste (Mungu, jalia lizififikie kanda!) na mkaungana katika dhehebu. Mungu kamwe hakulitaka Hilo liungane, Yeye alilitaka Hilo litenganishwe; kamwe lisiungane na ulimwengu.

116 Ibilisi yule yule wa kale aliyemfanya Hawa kutokuliamini Neno la Mungu na kumfanyia uovu, alirudi moja kwa moja na kuwachukua watoto wa Sethi na kuwafanya wawaone hawa wanawake warembo wa Kaini, nao wakaungana tena. Wala hawakuwa makafiri. Hawakuwa ni wakomunisti. La, la. Walikuwa ni waaminio. Walisema, "Sasa, labda huenda Bwana akafanya jambo fulani." Ama, loo, hili namna ile. Wao—walikuwa . . . Walidhania walikuwa wakifanya lililokuwa sahihi. Ndipo ikambidi Mungu kufanya nini? Kukifagilia mbali kitu hicho chote, ilimbidi kukifagilia mbali kitu hicho chote. Chini ya muungano wa uongo! Ilimbidi kutuma mafuriko na kuangamiza kundi hilo lote. Hukumu iliujia muungano huo wa uongo. Hukumu iliipiga Edeni kwa sababu ya muungano wa uongo.

Sasa, hivi nyoka alikuwa na uzao? Aibu kwako.

117 Muungano wa uongo ulileta hukumu juu ya dunia, kwa Hawa na Adamu, katika Edeni. Nao muungano wa uongo ulisababisha mafuriko ya hukumu ya Mungu duniani kwa sababu kwamba binti za Kaini walichezeana kimahaba na wana wa Mungu, nao wakawatamani na kuungana pamoja tena. Haya basi. Muungano haramu, "Hakuna kitu kingaliweza kutukia." Mungu alifanya nini? Alikiangamiza kitu hicho chote, wote isipokuwa mzee wa thamani Nuhu na familia yake. Yeye . . . waliungana pamoja.

118 Na tena baada ya hayo, baada ya kifo cha Nuhu, na familia hiyo ya kiroho ya Nuhu, muda si muda wajua, watoto wa wanadamu walianza kutupiana macho tena. Walifanya nini? Walisema, "Sasa, sisi si makafiri, sote tunamwamini Mungu." Kwa hiyo wakamchukua jamaa fulani, kuwa kiongozi, askofu fulani mkuu jina lake Nimrodi, nao wakajenga mnara. Hawakuwa ni makafiri. Waliamini kulikuwako na Mbingu. Waliamini kulikuwako na kuzimu. Waliamini katika hukumu. Lakini watoto wa Mungu pamoja na binti za wanadamu, tena, nao wakajifanyia muungano, wa uongo, nao wakajenga kanisa kubwa la jimbo, dhehebu kubwa mno, na sehemu zingine zote zilikuwa kwa—kwa Babeli, zilikuwa zilipe ushuru kwake.

119 Nao wakasema, "Nitawaambia yale tunayoweza kufanya. Mnajua sisi ni werevu." Walipata wapi hekima hiyo? Kutoka kwa ibilisi. Hiyo ni hakika. Waliipata kutoka kwa ibilisi kama—kama vile Hawa alivyofanya. Waliipata kutoka kwa ibilisi. Kwa

hiyo wakasema, "Tutajijengea dhehebu, tutamfurahisha Mungu. Nami nitawaambia tutakalofanya, tutakuwa na vipandio vidogo. Tutakimbia juu tukaimbe na kushangilia pamoja na malaika, kisha turudi huku chini na kuishi jinsi tutakavyo." Ibilisi huyo angali anaishi. Mnaona? Ilikuwa ni kinyume na amri za Mungu. Hawakutii amri Zake. Mungu alifanya nini? Vema, walijenga mnara wa Babeli, uongo tena, kwa hiyo Mungu akawavuruga na kuwatenganisha.

120 Mungu aliwatenganisha tena kisha akamtuma mzee Ibrahimu mwenye haki, kasema, "Nitakuchukua tu na kufanya taifa kutoka kwako." Mungu aliwatenganisha. "Toka miongoni mwao, Ibrahimu, acha kila kitu nyuma." Na Mungu hakumbariki mpaka alipoacha kila kitu nyuma, Lutu alikuwa ndiye wa mwisho. "Toka nje, Ibrahimu, jitenge na wasioamini. Nami nitakuchukua na kufanya taifa kutoka kwako. Nitafanya watu watakaotii amri Zangu. Nitawapa nafasi nyingine."

121 Maskini mzee mwema Ibrahimu akaenda kuishi katika nchi ya ugeni. Hivyo ndivyo kila Ibrahimu hufanya, kukaa katika nchi ya ugeni. Nini? Akiamini ahadi iliyokuwa haiwezekani, tukinena kibinadamu. Unafikiri hao madaktari mamboleo wa Kaini wangalisema nini siku hiyo? "Whiu, jamani, mzee, umri wa miaka mia moja, ati atampata mtoto kwa mkewe, tisini? Loo, jambo la kimzaha jinsi gani!" Lakini Ibrahimu aliliamini Neno la Mungu. Na chochote kinyume nalo, alikiita kana kwamba hakikuwako.

122 Mabatizo haya yote ya uongo, mihemko ya uongo, mambo ya uongo yanayoendelea siku hizi, sema hayako, amini Neno la Mungu na uzidi kuendelea. Ni jiwe tu la kujikwaa kukuzuia usiyafikie yaliyo halisi. Hiyo ni kweli. Songeni mbele moja kwa moja, enyi watoto. Neno la Mungu, Mungu hulitimiza Neno Lake. Sijali ni mambo mangapi ya uongo ibilisi anayoyatupa huko nje, Mungu angali ana Neno la kweli na Yeye hulitimiza Hilo.

123 Ibrahimu aliita chochote kinyume, kibaya. Warumi, mlango wa 4, kama unaliandika. Ibrahimu aliita kila kitu kinyume na Neno la Mungu kana kwamba hakikuwepo. Hiyo ni kweli. Yeye alimwamini Mungu, alitiwa nguvu, haijalishi mwili wake ulivyokuwa dhaifu, jinsi lilivyoonekana halikuwa linaenda kutukia, Ibrahimu aliendelea kuamini. Sasa, haikumlazimu kushuka madhabahuni na kusema, "Endapo haliji sasa hivi, nitafanya . . . Sijui kama niliamini ama la." Ibrahimu alidumu nalo kwa muda wa miaka ishirini na mitano kabla halijaja, bali lilifika kule. Daima hufanya hivyo.

124 Ibrahimu, akaja Isaka; Isaka, akaja Yakobo; kutoka kwa Yakobo wakaja wale wazee wetu; kutoka kwa wazee wetu, wakaingia Misri; huko Misri, wakawa taifa. Ndipo wakati alipolikuza taifa Lake, mafanikio Yake, Yeye alifanya nini? Mungu aliwatenganisha tena. Kutokuamini na imani

haviwezi kuenda pamoja. La, bwana. Yeye aliwatenganisha tena, kwa ajili ya walio Wake Mwenyewe. Yeye aliwafanyia nini kuhakikisha kwamba waliongozwa vema? Sikilizeni kwa makini sasa, hatuna muda mwingi sana sasa, labda dakika zingine kumi na tano. Aliwaongoza karibu. Angalieni, Yeye akaliinua taifa, akawaweka chini ya walimu na kadhalika. Walipigwa na wakalia, na kulia na kuendelea. Lakini Mungu alikuwa akiangalia chini, Yeye aliikumbuka kila ahadi aliyompa Ibrahimu. Siku moja Yeye—Yeye aliwazia . . . Aliwafanyia nini? Alifanya nini hapo Yeye alipowatenganisha? Aliwapa sheria na akawapa nabii, akawapa Nguzo ya Moto. Alifanya nini? (Ee Mungu!) Aliliweka kanisa Lake katika utaratibu. Nguzo ya Moto, Roho, kuwaongoza, nabii ambaye angewaambia Ukweli wa Neno Lake. Ndiposa wakawa tayari kwa ajili ya safari. Si ni ajabu hiyo?

125 Wakatoka na kuingia nyikani, wakifanya ishara na maajabu, wakifungua Bahari ya Shamu, wakiyaita mapigo ya kuzimu kushuka juu ya Farao. Loo, jamani! Nguzo ya Moto ikiwatangulia, amina, iliwaongoza usiku na mchana. Haleluya! Nabii, mkweli kwa Neno hilo, akisimama pale akiwanyosha. Amina. Alikuwa tayari kuwachukua watoto Wake basi. Hiyo ilikuwa ndiyo mara ya kwanza waliyopata kuitwa kanisa. Ilikuwa ni mfano wa yale Yeye anayoenda kufanya katika siku za mwisho. Tutalifikia hilo tena katika dakika moja tu. Aliwaita watoke, akawapa torati, akawapa Neno Lake, akawapa nabii, Yeye akawapa ishara, na Yeye akawatuma nyikani. Akawatenganisha na ulimwengu mwingine.

126 Wao walifanya nini? Waliwaona wanawake warembo wa Moabu, kanisa vuguvugu lenye miungu na miungu wa kike na kila kitu kingine. Wao walifanya nini? Wakawaandama, wakaoa miongoni mwao. Hiyo ni kweli, kweli kabisa. Ninawazia maskini hao wanawake warembo wa Moabu walikuwa ni warembo kweli.

127 Ninao unabii uliowekwa nyumbani, moja ya siku hizi nitausoma. Nanyi mnashangaa ni kwa nini ninawakemea wanawake jinsi nifanyavyo. Miaka thelathini iliyopita . . . Nina BWANA ASEMA HIVI! Miaka thelathini iliyopita wakati nilipoingia hudumani, Yeye aliniambia ya kwamba mwenendo wa wanawake ungekuwa mtovu wa maadili sana na kuhusishwa na siku za mwisho wangekuwa ndio kitu kilichochafuka kuliko vyote duniani. Kweli! Mwanamke alilianzisha hapo mwanzo naye Shetani anamtumia wakati wa mwisho. Basi angalieni kinachotukia, angalieni kote katika miaka. Kasema, "Ataendelea kujivua nguo." Kisha kasema, "Kutakuwako tu na kundi dogo sana, la Wateule wenyewe ambao wamekusudiwa tangu zamani, watakaoepuka hayo."

128 Wakati hilo ono lilipokuja, hilo lilinitia wasiwasi. Nikawaza, "Wanawake . . . " Nikafungua tena katika Biblia katika Isaya,

ninaamini mlango wa 5, na Hiyo ilisema, "Tawi ambalo limeepuka kutoka . . . binti za Sayuni, katika siku hiyo litakuwa la kupendeza kwa Bwana."

129 Mwanamke mmoja aliniandikia swali hivi majuzi, akasema, "Ndugu Branham!" Ama, la, ilikuwa ni mwanamume, mhudumu. Huenda amesimama hapa asubuhi ya leo. Anatoka tu Ohio. Naye akasema, "Tunataka kusema jambo lile lile unalosema, lakini tulipata jambo fulani kwenye kanda zako ambalo si sahihi." Kwa hiyo Billy akaniletea hiyo barua. Kasema, "Jambo fulani kwenye kanda zako," kasema, "linahitilafiana sana, Ndugu Branham, na Neno la Mungu. Na sisi tunataka—sisi tunataka kunena mamoja." Kasema, "Swali moja ninalotaka kukuuliza, hilo ni Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11, nalo linasema hivyo juu ya kifuniko cha kichwa cha wanawake, na wanaume wasiwe na kifuniko." Kasema, "Tunaamini hilo. Wanawake wanapaswa kuvaa kofia kanisani, nao wanaume wanapaswa kutoa kofia zao kanisani." Kasema, "Tunaamini vifuniko hivyo vya kichwa, na kadhalika." Kisha kasema, "Halafu swali lingine ni kwamba watu wanakuja kwetu na kusema Malaika wa Bwana hukuambia kila kitu. Kila neno usemalo linatoka kwa Malaika wa Bwana. Na, Ndugu Branham, ni vigumu sana kupigana na kitu kama hicho," kasema, "kanisani mwangu." Kasema, "Tunataka kunena mamoja. Sasa, Ndugu Branham, hivi huamini kwamba ulikuwa katika kosa dogo hapo?"

130 Nikamjibu, "Ndugu yangu wa thamani, siko makosani. Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11, ilisema mwanamke anapaswa kukifunika kichwa chake, na ni kwa nini. Kisha kifungu cha 15 kikasema amepewa nywele ndefu ziwe kama kifuniko, si kofia." Roho hiyo ya Ukatoliki ililitawala kanisa muda mrefu kutosha. Nywele zake ndefu ndizo kifuniko chake. Hivi si maumbile yenyewe . . .

131 Tena tazameni, ndipo basi hilo swali likarudi, mtu fulani aliniuliza wakati fulani uliopita . . . Nitalielezea wakati nikiwa nikilizungumzia. Akasema, "Vema, Biblia ilisema ya kwamba anapaswa kuwa na nywele ndefu kwa sababu ya malaika. Kwani malaika wana uhusiano gani na mwanamke?"

132 Nikasema, "Kwani malaika ni nini? Ni mjumbe." Paulo anasema nini? Kama mjumbe wa kweli, malaika kutoka kwa Mungu akija, afadhali uwe na nywele ndefu. Yeye atakihukumu kitu hicho. Hiyo ni kweli. Ni wangapi walio . . . wanaojua ya kwamba malaika ni mjumbe? Kweli kabisa. Mjumbe aliyetumwa kutoka kwa Mungu atalihukumu. Kasema, "Afadhali uwe na nywele ndefu, kwa sababu ya malaika." Hao wajumbe waliotumwa kutoka kwa Mungu wakija, watakihukumu kitu hicho. Naam, kweli, kwa sababu, mjumbe halisi kutoka kwa Mungu, malaika ana uhusiano na Mungu, nalo Neno Lake haliwezi kushindwa. Hiyo ni kweli kabisa. Mtakatifu Paulo

alisema pale, ya kwamba ikiwa hata Malaika kutoka Mbinguni akija na kufundisha lingine lolote, na alaaniwe. Hiyo ni kweli. Sasa tunaona ya kwamba hiyo ni kweli, anapaswa kuwa na nywele ndefu, hicho ndicho kifuniko chake.

133 Lakini ninawazia hawa wanawake warembo wa Moabu walikuwa ni warembo sana, huenda walikuwa wamejipamba kama baadhi ya Mayezebeli mamboleo wa siku hizi. Lakini, hata hivyo, sio wanawake wote! Nafikiri mwanamke aliye halisi ni kito cha thamani. Mungu asifiwe kwa ajili ya mwanamke aliye halisi. Ninyi ni wajakazi wa Mungu. Lakini mwanamke halisi ni kama mwanamume halisi, watalifuata Neno la Mungu bila kujali yale ibilisi asemayo, ama kitu chochote cha uongo.

134 Na kusema, "Mchungaji wetu alisema ni sawa kufanya *hivi*." Sijali yale mchungaji wenu aliyosema. Kama ni kinyume na Neno la Mungu, neno lake na liwe uongo, na ulitii Neno la Mungu. Sijali ni dhehebu gani ama yeye ni nini, iwapo ana lolote la kusema juu yake, mwambie aangalie kwenye Neno la Mungu. Kweli kabisa.

135 Loo, jinsi tungaliweza kwenda chini na kuona Mungu akiwatenganisha. Itatubidi kusimama kwa dakika moja tu. Ninayo Maandiko fulani hapa ninayotaka tu kuyaruka, kupata, tuharakishe tupate kufikia mwisho. Ndipo wakati... ilikuwaje wakati Yeye alipochukua mahali pale, wakati wale wanawake wa Moabu? Ilimbidi Mungu kuwatenganisha tena. Yeye alifanyaje?

136 Ndipo akaja Yesu. Sasa ambapo tunafikia mahali fulani. Ndipo akaja Yesu, ile chapa ya nafsi ya Mungu, uzao wa mwanamke, uliozaliwa na Mungu Mwenyewe. Yule Msanifu mkuu akajijengea Mwenyewe mwili. Haikumbidi kuomba mbao zozote kutoka kwa mtu yeyote, kutoka kwa mwanamke au mwanamume. Yeye alijijengea Mwenyewe nyumba. Loo, jamani!

137 Nawazia juu ya Stefano kwenye ile siku wakati yeye aliposimama, kasema, "Ninyi msiotahiriwa mioyo na masikio, ninyi wenye shingo ngumu. Sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu. Kama vile baba zenu walivyofanya, nanyi mnafanya vivyo hivyo!" Kasema, "Sulemani alimjengea Yeye nyumba, ila aliye Juu Sana hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono, lakini mwili umeuandaa Wewe."

138 Haikumbidi kuomba mbao zozote mahali popote. Waebrania, mlango wa 11, ninaamini katika kifungu cha 2 ama cha 3, inasema kwamba, "Ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu, hivyo vitu vilifanywa kutokana na vitu visivyo dhahiri." Mungu alisema tu, "Na iwe," na ikawa. Haikumbidi kwenda kule na kusema, "Bw. Mwezi, ungenikopesha mbao kidogo? Bw. Nyota, ungeniruhusu nichukue kalisi kidogo?" Mungu hafanyi hivyo.

139 Haikumbidi kusema, "Mariamu, nikopeshe yai, ninataka kufanya mwili nipate kuishi ndani yake." Mungu Muumba alinena, naye akawa mama papo hapo. Hakuwa ni mama, alikuwa ni mwanamke tu akiubeba Uzao Wake. Hiyo ni kweli. Kumbukeni, Yeye hakuwa mama wa Yesu. Ulimwengu ulisema hivyo. Nitafutieni mahali pamoja katika Maandiko ambapo Yeye aliwahi kumwita mama. Sasa rudini kwenye Neno. Ati "Mama wa Mungu," aibu kwenu. Mnaona?

140 Siku moja kulikuwa na watu waliomwambia, kasema, "Mama yako yuko nje akikutafuta."

141 Yeye akasema, "Mama Yangu ni nani?" Akawaangalia wanafunzi Wake, kasema, "Wale wayafanyayo mapenzi ya Baba Yangu ndio mama Yangu."

142 Yeye hakuwa mama Yake, alikuwa ni kiangulio. Mungu angaliweza kutumia kitu kingine, lakini Yeye alitaka kuchukua kilicho duni sana kuonyesha kile Yeye angeweza kufanya nacho. Akiinue, afanye kitu fulani kutoka kwa kilicho bure, huyo ni Mungu.

143 Ile chapa kamili ikaja, Yesu, Yeye asiye na dhambi, Yule mpendwa, aliye mzuri sana wa elfu kumi, Nyinyoro ya Bondeni, Waridi wa Uwandani, loo, Nyota ya Asubuhi. Yeye alikuwa ni nini? Alikuja kwa sababu gani? Sikilizeni kwa makini sasa. Kuimarisha tena umoja kati ya Mungu na mwanadamu. Loo, unaliona, ndugu?

144 Minara yao yote ya Babeli na mambo yao mengine yote huko nyuma hayakufanya kazi. Matunda yao yote ya bustani na vitu vingine vyote havikumpendeza Mungu. Kwa hiyo Mungu akashuka naye akachukuliwa mimba katika tumbo la uzazi la mwanamke, kwa Nafsi Yake Mwenyewe, akajifanyia Mwenyewe mwili, kisha akawa Imanueli, Mungu pamoja nasi; sio Myahudi wala Mmataifa, bali Mungu. Yeye hakuwa Myahudi, hakuwa Mmataifa, alikuwa ni Mungu. Nao Mataifa aliwapenda vivyo hivyo wakati wowote, ila tu Yeye alijaribu kumtenga Myahudi kama taifa. Alijaribu kufanya kila kitu kulirejesha, na jinsi pekee angaliweza kulianzisha ilikuwa ni kurudi kwa mtu binafsi kama Yeye alivyokuwa hapo mwanzo. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, kwa mtu binafsi. Si kwa dhehebu, si kwa shirika, si kwa kundi la watu; bali kwa mtu binafsi. Angalia, kuimarisha tena umoja kati ya Mungu na mwanadamu.

145 Yeye alikuwa ni dhabihu halisi ya dhambi. Kondoo, mbuzi, na kadhalika, wasingeweza kuondoa dhambi. Lakini ule uhai . . . Kwa sababu wakati dhabihu imechinjwa na uhai wa mwanakondoo, kitu kisicho na hatia sana, usingeweza kurudi, uhai huo, juu ya mwaminio, kwa sababu yeye alikuwa ni mwanadamu, aliye na nafsi, naye kondoo hana nafsi.

146 Mnaona, hakuna kitu kilicho na nafsi ila mwanadamu. Mungu aliweka . . . Yeye ni mfano wa mnyama, hiyo ni kweli,

bali Yeye aliweka nafsi ndani yake. Hicho ndicho kilichomfanya tofauti na wanyama. Yeye alijua mema na mabaya hapo nafsi yake ilipomjia. Lakini yeye. . .Kumbukeni wakati Mungu alipomuumba mwanadamu katika mfano Wake Mwenyewe, na kisha akawa nafsi iliyo hai. Mnaona, akawa hivyo, akijua mema na mabaya.

147 Sasa angalia. Lakini sasa, katika jambo hili, Yesu alikuja na Yeye alikuwa ni Mungu. Sio kwamba tu uhai wa mtu mwingine unaweza kumrudia mtu mwingine, bali Uzima wenyewe wa Mungu, ukimfanya mtoto wa Mungu, ukimrudisha katika muungano ule ule aliokuwamo kabla ya kule kuanguka. Sasa tunaupata ule umoja halisi.

148 Watu, mtu fulani ananiambia, "Ndugu Branham, hivi wewe si wa umoja?" Sio dhehebu la Umoja. Lakini mimi ni umoja na Kristo, mnaona, bali sio dhehebu la Umoja.

149 Yeye alilipa deni ya dhambi. Sasa, kusudi tupate umoja kati ya Mungu na mwanadamu, Yesu asingeweza kulifanya mradi tu Yeye alikuwa hapa katika mwili wa nyama. Kwa hiyo ilibidi awe dhabihu kamilifu ya dhambi apate kuiondoa hatia ya mwaminio, mnaona, kuiondoa kusudi Roho Mtakatifu aweze kuingia ndani ya mwanadamu, na kumfanya mwanadamu na Mungu umoja tena. Mnaona, ilibidi kuweko na kitu fulani cha kuanzisha tena.

150 Sasa, ni kitu gani kingaliweza kuanzisha tena? Amri ya Mungu inapotimizwa. Malaika angeweza kuitimiza? Yeye hana damu. Mungu angaliweza kuitimiza? Yeye hakuwa na damu. Basi Mungu akawa mwili na damu, kusudi aweze kulipa deni vizuri na kuondoa dhambi, kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee. Minara ya Babeli ikiwatenganisha kote duniani, kila kitu kingine, madhehebu na kadhalika yalikuwa yameshindwa kwa kila njia, yalichanganyikana, ulimwengu na kila kitu kingine, lakini huu ulikuwa unaenda kuwa ni utengano mkamilifu. Utukufu!

151 Sasa ninajisikia kubarikiwa. Vema, najisikia kana kwamba ninaweza kuchukua fungu langu sasa na kuanza kuhubiri sasa hivi. Ninapata joto tu sasa kufikia ambapo ninaweza kuanza papa hapa, na ni wakati wangu wa kufunga. Uhum! Labda nitaumaliza baadaye wakati fulani, umoja wa Mungu na mwanadamu. Je, mnaelewa? Wote wanaoelewa, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

152 Mnaona, hiyo ndiyo njia pekee ambayo mwanadamu angeweza kurudi katika ile hali yake ya asili tena, ni kwa adhabu hiyo ya dhambi kulipwa. Adhabu ya dhambi ni nini? Mauti. "Mshahara wa dhambi ni mauti." Naye Mungu alisema, "Siku utakayokula hilo, siku utakapofanya tendo hili, hiyo ndiyo siku utakayokufa." Basi lilipotendeka, liliuvunja uhusiano wake, ushirika na kila kitu kwa ajili ya mwanadamu, wala usingerudi tena mpaka adhabu hiyo ilipolipiwa. Na hakuna mtu aliyestahili kuilipia, kwa sababu kila kimoja kilianguka pamoja

na mwanadamu, maana kila kiumbe kiko chini ya binadamu, naye alikuwa ameanguka. Utukufu! Loo, ndugu!

153 Ndugu Mac, sikukuona umeketi hapo, Mungu akubariki. Tunaliamini hili, Ndugu Mac. "Kuja chini ya adhabu ya mauti." Ndugu Mac hapa alikuwa mchungaji hapa maskanini wakati nilipoondoka. Naam. Sasa, maskini mzee mwingine Mbaptisti mwema, Mbaptisti wa Kimishenari huko chini aliye na Roho Mtakatifu. Mnaona? Angalieni sasa, kuwa katika umoja na Mungu.

154 Sasa, tunapoliona hili, kuona ile adhabu haina budi kulipiwa, na kuona, umbile lililo juu sana la uhai wa mnyama ni mwanadamu, naye mwanadamu alianguka, mwenyewe. Kwa hiyo mwanadamu mmoja anawezaje kumwokoa mwingine? Ilimhitaji Mungu. Naye Mungu, katika Roho, asingeweza kufa. Kwa hiyo, "Ilimbidi Mungu kujishusha Mwenyewe chini kidogo kuliko Malaika," Waebrania mlango wa kwanza, kifungu cha kwanza. Ilimbidi kujishusha Mwenyewe chini kidogo kuliko Malaika kusudi ayachukue mauti, apate kulipia adhabu, kuleta umoja kati ya mwanadamu na Mungu tena, kusudi Roho Mtakatifu aweze kurudi.

155 Deni ya dhambi ililipwa. Ilimbidi Yesu kufanya hivi apate kumtuma Ro—Ro—Roho Mtakatifu tena juu yao, kuwaunganisha watu tena kama ilivyokuwa katika Bustani ya Edeni. Deni ililipwa wakati Yesu alipokufa. Hilo lilitosha. Amina, ndugu! Laiti ningalililifanya tu lizame ndani, mnaona. Deni imelipwa. Haleluya kwa Mwana-kondoo! Deni imelipwa. Na kila mwanamume na mwanamke anayenisikia asubuhi ya leo, ama atakayenisikia kwa kanda, adhabu yako imelipwa. Usikose kuliamini Neno la Mungu tena. Rudi kwenye Neno! Usiamini. . . Yeye alikuwa ni Neno. Utukufu! Ninajisikia kama kupiga mayowe, kweli ninajisikia. Adhabu imelipwa. Yote imekwisha. Si ajabu Malaika walipiga mayowe na kuimba, nyimbo za Mbinguni ziliimbwa. Naam, bwana, kondoo aliyepotea alipatikana! Upatanisho ulifanywa kwa ajili yake apate kurudishwa tena, maji ya farakano, Neno la Mungu linalomsafisha na uovu wake, wakati Neno lilipokufa mahali pangu kisha likafufuka tena na kuchukua ukuu maishani mwangu, moyoni mwangu. Amina. Adhabu imelipwa! Imekwisha. Tumekombolewa.

156 Sio na kanisa Katoliki; ingawa sisi ndio katoliki ya kweli, katoliki ya kimitume. Naam, bwana. Sio Katoliki ya Kirumi pamoja na mafundisho yao ya sharti, wao wanalikana Neno hili pamoja na fundisho lao la sharti; kila kitu ni fundisho lenu la sharti, sio Neno. Methodisti, Baptisti, aibu kwenu, wapendao maovu kuliko kumpenda Mungu. Wapendao anasa, watafuta ulimwengu, anasa, nguruwe waliochinjwa kwa ajili ya kizimba. Ibilisi anavituma vyombo vyake huko nje vikishindilia kitu hicho ndani yako kama vile Shetani alivyofanya katika

bustani ya Edeni. "Vema, wahudumu wetu wote wana elimu. Wanayo Ph.D., LL.D." Hilo halimaanishi kitu. Ukilikana Neno hilo, ungali ni ujanja wa ibilisi. Nimewathibitishieni kwa Neno asubuhi ya leo, ni juu yenu tangu sasa na kuendelea.

157 Wale wanafunzi, hata wakitembea pamoja na Yesu, hawakuwa na umoja. Hawakuwa na umoja wowote. La, walibishana, "Ni nani atakayekuwa askofu baada ya haya. Ni nani aliye mkuu zaidi miongoni mwetu?" Hata wasingemwamini Yesu. Wasingeweza kumwelewa. "Unazungumza katika mafumbo. Twambie dhahiri unayomaanisha." Hapakuwapo na umoja kati ya Yesu na wale wanafunzi, ama wanafunzi kwa Yesu, na wanafunzi miongoni mwao wenyewe.

158 Haidhuru, hilo linakuonyesha, ndugu. Sikilizeni kwa makini sasa, ninataka hili lishike sana kwenye kilindi cha moyo wako. Mnaona? Mungu anao mpango. Nje ya mpango huo, sijali ni hekima kiasi gani iliyo nyuma yake, ni mamilioni mangapi mazuri ya dola ya mijengo, ni shule ngapi za theolojia, ni watu wangapi watakatifu na *hili* takatifu, na takatifu, takatifu, takatifu, haileti tofauti hata kidogo, ikiwa Neno moja la Biblia ya Mungu limekanwa, ni ya ibilisi. Sasa, nimewathibitishia hilo kwa Neno la Mungu lililoandikwa, kutoka kwenye Agano Jipya hata la Kale, nami nitalishusha chini kufikia siku hii kama tu mtaketi pamoja nami dakika chache.

159 Wanafunzi waliotembea moja kwa moja na Yesu, wakalala pamoja na Yeye, wakala pamoja na Yeye, wakaiangalia miujiza Yake, na kushirikiana Naye, kwa karibu kama ndugu yeyote angaliweza kuwa, na hata hivyo hawakuwa nao. Hawakustahili kuihubiri Injili. Yesu alisema, "Msihubiri tena, hata msijaribu. Ninyi ngojeni kule juu katika mji wa Yerusalemu. Nitaituma ile ahadi, ambayo mmepewa, juu yenu. Hiyo itawaunganisha basi."

160 "Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba watakuwa mmoja kama tu vile Wewe na Mimi tulivyo Mmoja. Nami . . ." "Kama vile Baba Yangu alivyonituma Mimi kuihubiri Injili, Mimi nami nawatuma ninyi."

161 Naye Baba mwenyewe aliyemtuma Mwana, alikuja ndani ya Mwana. Umoja kama Mmoja. Alisema, "Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini kama kazi nizifanyazo Mimi zinanena kwa sauti kubwa hivyo, ninyi ni viziwi kabisa, bubu na vipofu kama hamlioni." Loo, ndugu, whiu! Kasema, "Enyi wanafiki! Mnaweza kuutambua uso wa anga, bali ishara za wakati hamwezi kuzitambua. Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua na siku Yangu. Isaya alinena vema juu yenu. Mnayo masikio, nanyi ni viziwi sana hamwezi kusikia. Macho, na ni vipofu sana hamwezi kuona!"

162 Mtume Paulo alisema vema, "Katika siku za mwisho watakuwa na mfano wa utauwa na kuzikana Nguvu zake," na Maandiko baada ya Maandiko, kile kingetukia katika

madhehebu haya katika siku za mwisho. Ndipo wanashangaa ni kwa nini ninapiga makelele dhidi ya mfumo huo wa kujibunia wa ibilisi. Watazame hao watoto wa thamani wakitegwa huko nje kama kondoo wakipelekwa machinjioni. Watoe, Bwana!

163 Naam, wanafunzi hawakuwa na umoja. Wasingeweza kumwelewa Yesu. Wao walisema, "Ai, ni nani anayeweza kuyafahamu mambo haya?" Mnaona, Mungu hakuwa ndani yao bado. Walikuwa tu wameshirikishwa katika ushirika. Walikuwa tu wameshirikiana na Yeye. Hao ni watu wengi wazuri siku hizi. Hawakunywa pombe, kusema uongo, kuiba, hawakufanya chochote, bali hawakuwa na umoja huo wa Mungu. Hawakuwa mmoja na Mungu bado. Mnaona, wasingeweza kuwa. Loo, walifanya miujiza. Walitoa pepo. Hiyo siyo ninii—hiyo siyo ninii . . .

164 Nilisoma makala katika gazeti hivi majuzi kuhusu hilo, kuhusu kutoa pepo. Watu wanasema, "Loo, ndugu, ninakwambia, hiyo ndiyo." Hiyo siyo! Mtu anayetoa pepo na kulikana Neno la Mungu, ni mwongo. Naam, bwana. Yeye husema anawatoa pepo. Wanadai wanafanya hivyo. Yeye hawezi kufanya hivyo kama hayuko pamoja na Neno la Mungu. Yesu alisema hivyo.

165 Sasa, ndipo ikaja Pentekoste, Mungu akawafanya mmoja tena. Loo, jamani! Ndipo walikuwa na umoja na Mungu. Mungu alikuwa ndani yao. Sasa, Matendo, kama unayaandika, Matendo 4:32, Biblia ilisema ya kwamba "Walikuwa na moyo mmoja, nafsi moja, na nia moja." Loo, ndugu. Kwa nini? Walikuwa wamerejeshwa kwenye ya asili tena. Kitu pekee walichokuwa wameacha cha kutupwa kilikuwa ni mji wa kale, ama waliishi hapa ndani, mwili wa kale unaoitwa mji ama hekalu, walioishi ndani yake hapa, ambao ulipaswa kuoza, kwa kuwa hauna budi kufa na kuharibika. Lakini katika roho na uzima, na katika kusudi na ono, na kila kitu, walikuwa mmoja na Mungu.

166 Loo, Adamu, rafiki yangu mwenye huzuni, usiache Shetani akwambie uongo wake tena. Usiache hilo litendeke. Usiache Shetani akwambie ya kwamba Neno halimaanishi yale lisemayo. Hiyo ni kweli. Neno linamaanisha . . . Naam, hapa sio . . .

167 Nilikuwa nikizungumza juu ya ubatizo wa Jina la Yesu Kristo. Hiyo ni kweli, ufunuo wa huo ulikuja. Hiyo ni Kweli. Lakini kundi la watu lilifanya nini? Lililikusanya pamoja hapa nje na kuweka dhehebu kutoka kwake, likafanya mnara mwingine wa Babeli. Jambo lile lile, likalitupa moja kwa moja ndani yake. Bila shaka. Luther alifanya jambo lile lile. Wesley alifanya jambo lile lile, John Smith alifanya jambo lile lile, Alexander Campbell alifanya jambo lile lile. Pentekoste ilifanya jambo lile lile. Mungu hujishughulisha na watu binafsi wanaolitii Neno Lake. Mpango wa pekee wa Mungu wa kuwaleta waaminio Kwake, katika umoja wa kweli, ni kumpokea Roho Mtakatifu. Basi hivi ndivyo . . .

168 Unasema, “Vema, Ndugu Branham, nilinena kwa lugha. Nilipaza sauti. Nilifanya *hivi*.” Kama ungali una roho ya namna hiyo na kulikana Neno la Mungu, huna Neno la Mungu ndani yako, huna Roho. Kama utaketi na kuisikia ile Kweli ikihubiriwa, nawe uiangalie Hiyo katika Biblia na kuona Hiyo ni Kweli, kisha ukatae kufanya hivyo, huyo si Roho wa Mungu. Sijali ni kiasi gani ulinena kwa lugha, jinsi ulivyopaza sauti, ni kiasi gani cha makanisa uliyokuwa mfuasi wake, ama ni mara ngapi ulibatizwa, ama chochote kingine. Neno ni Kweli. Hilo ndilo linaloithibitisha ile kweli. Kama unazo kweli hizi zingine zote halafu pamoja na Neno, amina, basi unajua unakuja nyumbani.

169 Unaweza. . .Mungu yule yule aliyeandika Biblia anawezaje kugeuka na kubadilisha Neno Lake na kitu kingine? Ninyi Wakatoliki mliosema ya kwamba Petro alizikwa kanisani mwenu, nayo roho yake inawapa haki ya kuziondoa dhambi na kadhalika, Petro angewezaje, Myahudi, kamwe kuvumilia kuwa na sanamu kanisani? Petro kamwe angewezaje kukataa kusema ya kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuja, naye alinena kwa lugha, na mambo hayo yote yenye nguvu aliyofanya, na kugeuka na kusema mle maskini mkate mwembamba, na Mungu yuko kwenye huo mkate mwembamba? Loo, ni ujinga, ujinga wa kiroho!

170 Vema, sasa, nyinyi Waprotestanti jambo lile lile, mnatembea na kupeana mikono na mhubiri, na kusema, “Ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu binafsi,” kisha mnarudi na kuishi maisha ya aina yoyote kwake, na kuendelea kuishi pamoja na ulimwengu. Mnara mwingine wa Babeli.

171 Tunashuka kuja kwenye mwisho sasa. Angalieni. Mungu alimtuma Roho Mtakatifu, naye Roho Mtakatifu ni Mungu Mwenyewe. Yeye Ndiye atakayefanya umoja kati ya Mungu na mwanadamu. Hebu tuchunguze. Sasa hebu. Sasa nataka usikivu wenu mkamilifu kwa dakika tano zijazo ama kitu kama hicho. Angalieni.

172 Mwanadamu chini ya mpango wa ibilisi amejaribu kuliundia kanisa dhebebu kuliingiza katika umoja. Wamejaribu kuunda dhehe-. . .kulielimisha kanisa liingie katika umoja, mwajua hilo, kupitia kwa elimu, kupitia kwa madhehebu. Wanajaribu sasa hivi, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, litakalowaleta Katoliki na Waprotestanti wote pamoja na kuwafanya mmoja. Ni kitu gani? Mpango wa ibilisi!

173 Mnasema, “Wewe ni mdogo sana kusema hilo.” Mimi ni mdogo sana, bali Neno la Mungu wangu ni kubwa mno, nitawaambia hilo. Mbingu na nchi zitapita, bali Hilo halitapita. Si yeye anayelisema, ni Yeye ndiye—Yeye ndiye—Yeye ndiye aliyelisema kwanza. Mimi ninasema tu yale Yeye aliyosema, ninalikiri Neno Lake.

174 Liko chini ya ibilisi! Limethibitishwa katika Neno hapa, papa hapa asubuhi hii mbele yenu, kwamba ni ya ibilisi. Lolote la madhehebu hayo liko hivyo. Watu, chini ya mpango wa ibilisi, wanajaribu kuwaundia watu dhehebu kuwaingiza katika umoja.

175 "Ninyi nyote njoni mkajiunge na Assemblies of God. Mkajiunge na Umoja. Jiungeni na Church of God. Jiungeni na Methodisti. Sisi sote ni mmoja." Enyi kundi la wanafiki, wenye mfano wa utauwa huku wakikana Nguvu Zake. Nalo Neno la Mungu linatikiswa papo hapo mbele zenu, nanyi mnaogopa kulishambulia. Mbona Mungu hajionyeshi Mwenyewe basi, iwapo mko na Mungu? Kwa nini hamzifanyi kazi za Mungu? Mnawezaje kuwa na mfano huo, na kwenda huku na huku na kumkana Yeye, hata kuziita kazi halisi za Mungu Beelizebuli? Inaonyesha, enyi kundi la kanisa lililoelimika! Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi!" Kweli! Nina hakika mnaelewa ninalomaanisha. Bila shaka. Kwa nini mtu fulani asilishambulie Hilo? Mnajua Mungu yuko nyuma Yake. Mungu atasonga na Neno Lake.

176 Mwanadamu hufanya hivyo, inajenga mnara mwingine wa Babeli. Yeye anafanya nini? Wanajaribu kuonyesha... Angalieni katika Baraza hili la Makanisa sasa. Waanglikana, Katoliki ya Kirumi, Methodisti, Presbiteri, Wapentekoste, na hao wote wameungana pamoja, Sayansi ya Kikristo, na mengi ya madhehebu ambayo hata yanakana kuzaliwa na bikira, wanaukana Uungu wa Yesu, kumfanya Yeye watu watatu, kujaribu kuwaabudu miungu watatu, kukana kuzaliwa na bikira. Wengine wao huikana Damu. Baadhi yao huikana miujiza Yake. Wote wanaikana, karibu wote. Halafu basi—halafu kujaribu kuwaunganisha kama hao pamoja, unawezaje kufanya hivyo? Ni mnara uliobuniwa na mwanadamu. Utaanguka kama Babeli ilivyoanguka.

177 Lakini Mungu alisema, "Si kwa uweza, si kwa nguvu; kwa Roho Yangu, asema Bwana. Hivyo ndivyo nitakavyoliunganisha Kanisa Langu. Sio kwa dhehebu, sio kwa elimu, sio kwa wanatheolojia; bali kwa Roho Yangu, asema Bwana, nitawaleta kondoo Wangu pamoja." Loo, jamani! Basi anapofanya hivyo, inakuwaje? Nazo ishara Zake zitashuhudia jambo lilo hilo. Hivyo ndivyo Israeli ingeweza kusema, kabla hawajachanganyikana na Moabu. Kulikuwako na Nguzo ya Moto juu yao. Naam, bwana. Atafanya nini? Atashuhudia, ushuhuda wa namna ile ile. Lakini walipojitenga na Mungu, wakautenganisha umoja wao kati yao na Mungu, na kuungana na Moabu na hao wengine, huo ushindi ulishindwa kabisa. Walikaa nyikani kwa muda wa miaka mingine arobaini, mpaka Mungu akaliinua kundi lingine kwenda huko na kukamilisha mpango Wake. Hivyo ndivyo walivyofanya hasa.

178 Sasa angalieni. Lakini wakati Mungu anapolileta kanisa pamoja kwa Roho Yake, watakuwa na ishara Zake za Mungu aliye hai miongoni mwao. Ishara za namna gani? Wakati Mungu alipowatenganisha Israeli kutoka Misri, Mungu alimpa Musa na Israeli ishara ya Nguzo ya Moto. Hiyo ni kweli? Nabii. Wakati alipomtenganisha Ibrahimu kutoka kwa Lutu, kulikuwako na Malaika aliyemjia, ambaye angeyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Ishara! Haleluya.

179 Sasa madhehebu haya yaliyonaswa katika kanisa hili, yakijaribu kufanya umoja kama huko Misri, kama huko chini katika—katika Edeni, na kadhalika, chini ya huu ushawishi mkuu waliomo.

180 Lakini, angalieni, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Wakati Mungu alipowatenganisha Israeli, Yeye aliwapa ishara ya Kimbinguni, Nguzo ya Moto. Yeye aliwapa nabii. Yeye alimfanyia nini Ibrahimu? Yeye hufanya nini kila wakati? Nionyeshe nabii aliyechaguliwa na Mungu miongoni mwao. Yeye aliliweka kanisa Lake pamoja kwa mitume na manabii na walimu na wainjilisti. Haleluya! Haya basi. Kanisa, tena, kama vile Yeye alivyowaita Israeli watoke. Niliwaambia ningelirudia. Naam, bwana.

181 Hakuna manabii waliochaguliwa na Mungu miongoni mwao, la, bwana, kama walivyokuwa pamoja na Israeli na hao wengine. Ni kitu gani? Mnara wa ibilisi tena.

182 Sasa, kule Kuja kumekaribia sana, kule Kuja kwa Pili kwa Yesu, Yeye anawakusanya Wateule Wake pamoja. Ninaamini hilo. Loo, watakuja kutoka Mashariki na Magharibi. Palipo na mzoga, tai watakusanyika. Loo, jamani, ni kitu gani? Yeye ana umoja Wake, umoja Wake wa kweli, akijionyesha Mwenyewe miongoni mwao; kutoka kwa kila dhehebu, akiwaleta Wateule Wake pamoja kutoka kila namna ya makanisa, kutoka kila mahali, akiwatoa watoto Wake, wakiingia moja kwa moja mstarini pamoja na Neno Lake. Kitu gani?

183 Sasa, Kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia sana, kule kuja kwa hukumu, Yeye anawaita Wateule Wake pamoja katika umoja na Yeye Mwenyewe, kwa aina ile ile ya huduma kama aliyokuwa nayo. Mnajua vile nilivyoziweka katika Nyakati za Kanisa, hapa si muda mrefu uliopita, kuhusu ule—ule mnara mkubwa uliojengwa, unaoitwa piramidi, bali jiwe la kichwa kamwe halikuwekwa juu yake. Kumbukeni jinsi Walutheri walivyokuja, kisha akina Wesley katika uchache, halafu kushuka kwenye Pentekoste. Na sasa yale Yeye anayofanya, kuita kutoka hao. Yeye alifanya nini? Aliwaita walio Wateule, kufanya Walutheri; Yeye akawaita Wateule, kutoka kwa Walutheri, kufanya Wawesley; Aliwaita Wateule, kutoka kwa hao, kufanya Wapentekoste; sasa Yeye anawaita wapentekoste Wateule watoke, kufanya jiwe la kichwa liingie ndani yake. Huduma ya namna ile ile ikishuka moja kwa moja ndani yake, akiwaita

watoto Wake kutoka kwa madhehebu yote na matabaka yote ya maisha.

184 Amefanya nini Yeye? Ameweka pamoja nao walimu wa kweli, manabii wa kweli ambao wanadumu na Neno Lake, Biblia. “Kondoo wangu huisikia Sauti Yangu,” kasema Yesu. Kama hiyo ilikuwa ni Sauti Yake wakati huo, ni Sauti Yake sasa. Kitu chochote kinyume na Sauti hiyo, si chakula cha kondoo. Hawatakifuata. Loo, ndugu. Kutoka Mashariki, kutoka Magharibi, kutoka kwa kila dhehebu, kutoka kwa kila shirika, wamekuja kutoka Mashariki na Magharibi, wakikusanyika pamoja! “Tutafanya karamu pamoja na Mfalme, tusherehekee kama wageni Wake, jinsi wasafiri hawa walivyobarikiwa! Wakiutazama uso Wake mtakatifu unaonawiri kwa upendo wa Kiungu; washiriki wabarikiwa wa neema Yake, watanawiri kama vito katika taji Yake. Yesu yuaja karibuni, majaribu yetu basi yatakwisha.” Haleluya! “Vipi kama Bwana wetu angekuja dakika hii kwa ajili ya walio huru na dhambi? Ndipo je, lingekupa furaha, ama huzuni na kukata tamaa sana? Bali Bwana wetu atakapokuja katika utukufu, tutamlaki Yeye juu hewani.” Haleluya! Naam, bwana.

185 Ni kitu gani? Pamoja na walimu waliotumwa na Mungu watakaodumu na Neno, kwa Kanisa halisi, pasipo kusonga hata chembe haidhuru dhehebu linasema nini. Hawajaunganishwa nalo. Manabii; sio kujifanya kuamini, wanavyojiita, bali nabii halisi ana BWANA ASEMA HIVI, na moja kwa moja kwenye alama kila wakati. Hilo ndilo amelituma Kanisani Mwake. Hivyo ndivyo Yeye alivyosema angefanya. Wanaliamini Neno; sio kanuni ya imani, sio fundisho la sharti, bali Neno. Na, kwa kufanya hivi, Yeye anajionyesha Mwenyewe ndani yao kwa kulithibitisha Neno Lake, akiyafanya Maisha yale yale Yeye aliyoishi wakati mmoja, kuishi tena, akilitimiza Neno Lake. Loo, jamani!

186 Sikilizeni kwa makini. Wakorintho wa Kwanza 4:20, inasema, “Ufalme wa Mungu ni Neno Lake lililofanyika nguvu.” Kama ukitaka kuandika hilo, Wakorintho wa Kwanza 4:20. Ufalme wa Mungu ni Neno la Mungu lililofanyika nguvu. Ufalme wa Mungu ni nini? Uko ndani yenu. Huo Ufalme uko ndani yenu. Ndipo Neno linapoingia mle, Neno hili linaanzisha nini? Linajigeuza Lenyewe likawa nguvu, zikilifanya Hilo liseme vile lilivyosema hasa.

187 Huwezi kusema “Linasema *hivi*,” na linasema Hivi, na kulifanya Hilo litende kazi. Inakubidi kusema jambo lile lile Hilo lisemalo. Hiyo inafanya maungamo. Sio kusema, “Vema, Hilo limepigwa msasa kidogo hapa, nitapata hekima zaidi, nitakuwa na msimamo mzuri zaidi huku.”

188 Wewe kaa na Neno. Hilo hapo, mnaona. Nalo linalifanya Hilo kuwa nguvu. “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Mkikaa ndani

Yangu na Maneno Yangu yakae ndani yenu." La, samahani, hivyo sivyo Yeye alivyosema hapo. Alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu, mwaweza kuomba mtakalo nanyi mtatendewa. Mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu."

189 Ni kitu gani? Inakubidi kuwa pamoja na Neno, wewe mwenyewe uuawe. Nimeshawishika ya kwamba wengi wetu, enyi marafiki, tumempokea Roho Mtakatifu, bali tunampokea tu Roho Mtakatifu wa kutosha ndani yetu kutufikisha mahali ambapo hatutaki kusema uongo, hatutaki kuiba, hatutaki kufanya lolote. Lakini Mungu anataka kujaza kila mshipa wa Kanisa Lake, Yeye anataka kujaza mawazo yako na anataka kujaza nia yako. Anataka kuijaza kila sehemu yako, kukufanya tu mfu kwelikweli, kabisa kwa nafsi yako ama kwa mawazo yako, umejitolea tu kabisa katika Mungu mpaka Neno Lake linaishi tu moja kwa moja kupitia kwako. Hujui kitu kingine chochote ila Neno la Mungu, kudumu tu moja kwa moja na Neno Lake, Hilo ni Uzima. "Maneno Yangu ni Uzima," kasema Yesu. Aliweka pamoja nao, walimu walioiamini Biblia, manabii wanaosema Kweli, wanaosema, wanaoonyesha unabii ule ule ambao sikuzote wameuonyesha kote katika wakati. Yeye amefanya nini? Anajionyesha Mwenyewe hai miongoni mwao, akilithibitisha Neno Lake. Neno Lake, Ufalme wa Mungu ni Neno la Mungu lililofanywa nguvu.

190 Wakati, madhehebu haya yanategemea hoja za kibinadamu, juu ya hoja za kibinadamu. Sikilizeni kwa makini sasa. Wao. . .Hatupaswi kutegemea hoja za kibinadamu. Methali, mlango wa 3, kifungu cha 5, ilisema, "Usitegemee akili zako mwenyewe." Mnaona? Msifanye hivyo, haidhuru Neno la Mungu *linaonekanaje*.

191 Unasema, "Vema, linaonekana kana kwamba ni zuri tu *hivi*."

192 Hivyo sivyo Hilo lilivyo. Ni Neno la Mungu, lichukue jinsi Yeye alivyolisema. Hawa alisema . . . Shetani alimwambia Hawa, "Ninajua Mungu alisema Hilo, bali Hilo kweli halimaanishi hivyo. Linamaanisha hivi." Naye akaliamini. Akaliamini. Hiyo iliuvunja ule umoja, hiyo iliuvunja ule ushirika, hiyo iliuvunja ule muungano, hiyo iliuvunja ulimwengu, hiyo iliuvunja uhai, hiyo ilivunja kila kitu!

193 Naye mtu asiyeliamini Neno moja la Neno la Mungu, hilo linavunja ushirika wote na yote. Kweli! Tunaliamini Hilo ama hatuliamini. Hebu tudumu Nalo! Mungu alisema hivyo, basi hebu tukae na Hilo. Mambo mengi sina budi kuyaruka hapa, maana wakati umepita tayari.

194 Kama katika nyakati zilizopita, katika nyakati zilizopita wakati mwanadamu alipofanya hivi, ilileta hukumu ya Mungu

kwa ulimwengu. Ule mnara wa Babeli, muungano wa watoto wa Kaini pamoja na watoto wa Sethi, ulileta hukumu. Daima huleta hukumu ya Mungu kwa ulimwengu. Mnaona? Loo, umoja wa kweli na Yeye utainuka katika hukumu, juu yake, kama vile Nuhu alivyofanya katika ile hukumu pamoja na familia yake. Nuhu mwenye haki na familia yake walienda juu ya zile hukumu. Walifanya nini? Walienda!

195 Ndugu Lee Vayle, ukilipata hili, hili hapa. Hilo ndilo swali pekee tunalokosa kukubaliana juu yake, yeye anaamini Kanisa litapitia kwenye hukumu. Silioni hilo. Siamini hilo.

196 Nuhu kamwe hakupitia kwenye hukumu zozote, yeye alienda juu ya hizo hukumu. Ibrahimu kamwe hakuwa na moto wowote, alikuwa nje ya ule moto. Israeli hawakuwa katika zile hukumu za Israeli, walitenganishwa kutoka kwenye huo moto, kutoka kwenye hizo hukumu. Kanisa litaabiri juu ya hukumu, katika safina ya Roho Mtakatifu, limeinuliwa juu kutoka ardhini.

197 Kitu hiki cha Baraza la Makanisa si kitu kingine ulimwenguni bali ni ku—kuchochewa kwa yule mwanamwali mpumbavu, kuachwa hapa duniani wapate kuwindwa na mpinga-Kristo. Lakini Kanisa halisi la Mungu litaelea kama mzee Nuhu alivyofanya, na liende Utukufuni kwa hakika tu kama ninavyosimama hapa. Hiyo ndiyo sababu Yeye anawakusanya pamoja. Hilo ndilo ile Sauti inanena siku hizi. Hilo ndilo Mungu analofanya, ni kukusanya mmoja kutoka Los Angeles, na mmoja kutoka Filadelfia, na mmoja kutoka Georgia, na kadhalika. Kuwakusanya pamoja, watu Wake walio tayari kuliamini Neno la Mungu aliye hai. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, ambapo wachache waliokolewa, wachache sana." Vema, safina yetu ya Roho Mtakatifu itaelea moja kwa moja juu ya hukumu za Mungu, maana tayari tumehukumiwa, tunapomkiri Yesu, na Yeye aliichukua hukumu yetu.

198 Madhehebu haya, hata hivyo, yana vichwa vigumu sana! Hayo ni kama Hawa, yeye alitaka hekima yake bila kujali kile Neno la Mungu lilichokuwa. Nimrodi alitaka mnara wake, bila kujali, Maandiko ama la! Walikuwa vichwa vigumu! Hawa alijua vema zaidi. Sethi alijua vema kuliko kuvutiwa na hao wanawake warembo. Israeli ilijua vema kuliko kutoka nje huko katika uzinzi. Nanyi pia! Lakini wengine wana vichwa vigumu sana, yawe ni Maandiko ama si Maandiko! "Mungu abarikiwe, mama yangu alikuwa ni Mpresbiteri! Nitakuwa huko, pia." Endelea, kuendelea ndilo jambo la pekee unaloweza kufanya basi. Mungu airehemu nafsi yako yenye dhambi. Utaiepukaje, wakati unajua kwamba ni kweli? Na kama ukiliona Neno la Mungu, na ungali hudhani Hilo ni Kweli, basi kuna kasoro na upambanuzi wako wa kiroho. Hiyo ni kweli kabisa. Tazameni kote nchini muone ambako mambo haya yanatukia. Tuko kwenye wakati

wa mwisho, enyi marafiki. Hivi ndio kwanza tupitie kwenye Nyakati za Kanisa na kujua yatakayotukia katika wakati wa Kanisa la Laodikia? Hivi si ndio kwanza tupitie hayo? Mnaona ninalomaanisha? Tuko kwenye wakati wa mwisho.

199 Mungu anawakusanya Wateule kutoka kwenye pepo nne za dunia. Yeye alisema angewatuma malaika na kuwakusanya. Hiyo ni kweli? Kuwakusanya pamoja, awatenganishe na makapi. Amina. Makapi yatateketezwa, sio ngano. Kweli.

200 Lakini, wao wana kichwa kigumu sana, walipate wasilipate, haileti tofauti yoyote. Loo!

201 Lakini Waliochaguliwa wa Mungu wameamriwa kutoka miongoni mwao. "Mkatengwe nao," asema Mungu, "na Mimi nitawapokea. Msiviguse vitu vyao vya kilimwengu, na Mimi nitakuwa Baba kwenu, ama Mungu, nanyi mtakuwa wana na binti Zangu. Msijifunge nira pamoja na wasioamini, bali tokeni kwake!" Mungu anataka utengano kutoka kwa ulimwengu. Anataka kuungana pamoja na wewe, Yeye Mwenyewe. Wala hakuna mpango wa kujibunia wa shirika, dhehebu, ama nadharia zozote zilizobuniwa na wanadamu zitakazosimama kamwe. Itahitaji Mungu, Roho Mtakatifu, ndani yako, kukuunganisha na Mungu. Nawe unajuaje kwamba unaye Huyo? Roho Mtakatifu aliyeliandika Neno atalishuhudia kila Neno; na mambo yale yale ambayo Roho Mtakatifu aliyafanya katika Agano la Kale, Yeye atayafanya katika Agano Jipya; atafanya sasa vile vile, kwa sababu Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nawe hujafungwa nira pamoja na madhehebu na ulimwengu. Hujafungwa nira pamoja nao. Usijifunge nira miongoni mwao, bali toka miongoni mwao! Umefungwa nira pamoja na Kristo. Amina. Umefungwa nira kwa Bwana Yesu Kristo.

202 Biblia inasema, katika siku za mwisho kutakuwa na makanisa, mnara mwingine kama wa Babeli. Watakuwa na mfano wa utauwa, na kulikana Neno la Mungu pamoja na Nguvu, Nguvu za Neno Lake. Nalo Neno ni nini? Ufalme wa Mungu ni nini? Hatuna budi kuwa wa huo Ufalme kabla hatujaweza kuwa raia wa Mfalme. Ni wangapi wanaojua hilo, semeni "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, unaingiaje katika Ufalme huo? Ufalme wa Mungu ni Neno la Mungu lililorejeshwa katika nguvu. Amina. Lililofanywa nguvu; likiondolea mbali dhambi, likitoa ishara. Ishara ya aina gani? Ikiwa ni Neno lile lile lililomtoa Musa nje, litaleta ishara ile ile.

203 Kitu kile kile kilichomtenganisha Lutu vuguvugu. Sasa, tunajua Lutu alikuwa vuguvugu, naye Yesu alisema hiyo itakuwa ndiyo ishara ya wakati wa mwisho. Lutu vuguvugu akiketi huko ng'ambo, alikuwa wa kidini, hakika, yeye na mke wake. Nao walikuwa wanachama wa kila namna ya vyama, naye alikuwa ndiye meya wa huo mji, na, loo, kulikuwako na mambo chungu nzima yaliyokuwa yakiendelea. Yeye alikuwa ni wa kidini sana.

Angeweza kuwaburudisha wainjilisti na wote waliopitia kule, alikuwa sawa hivyo. Lakini, loo, ndugu, yeye hakuwa ni yule Mteule.

204 Angalieni lililotukia! Kwa nini? Mungu yeye yule aliyewatenganisha kisha akamjia Ibrahimu na kumwonyesha thibitisho la utengano wake. . .Uhum! Ee Mungu! Laiti ningalininii—laiti ningaliweza tu kufanya jambo fulani kuwafanya mlione Hilo. Mungu alimwonyesha Ibrahimu, kwa kuwa alikuwa amejitenga mwenyewe, Yeye alimwonyesha thibitisho lake, kwamba Yeye alikuwa pamoja naye na papo hapo miongoni mwake. Naye Yesu alisema jambo lile lile litatukia katika siku za mwisho. Ibrahimu hakuwa taifa, yeye alikuwa katika uchache, lakini Mungu alikuwa pamoja naye. Yeye alikuwa amemtenganisha wakati huo. Tunapaswa kujitenga wenyewe katika hizi siku za mwisho.

205 Na kama Mungu alimpa Musa ishara, kwa Israeli, nabii aliyetiwa mafuta, Nguzo ya Moto, akampa Ibrahimu ishara. Yeye—Yeye aliwapa Israeli ishara. Akawapa wanafunzi ishara. Ishara ile ile, kila wakati! Ishara ile ile, Nguzo ya Moto!

206 Paulo, wakati alipokuwa akienda zake Dameski, Nguzo ya Moto iliangaza mbele zake, ambayo hata iliyapofusha macho yake, ikamwangusha magotini mwake. Hakuna mtu mwingine aliyeiona. Kila mtu aliyesimama hapo karibu, hawakuiona. Ndipo Sauti ikasema, "Sauli, mbona wanitesa?"

207 Akasema, "Bwana, U Nani Wewe?"

208 Akasema, "Mimi ni Yesu." Ishara! Naye alikuwa ni nini? Mtume kwa Mataifa. Amina.

209 Sisi hapa katika wakati wa mwisho, tukitoka Mashariki na Magharibi, Kaskazini na Kusini. Tunafanya nini? Tunajiweka tayari kwa ajili ya huo Unyakuo. Tunajiweka tayari kwa ajili ya. . .Tukijishikilia imara kwa dakika chache mpaka kila mshipa umejazwa na Roho Mtakatifu. Ndipo Hilo litapaa juu. Loo, jamani! Akiwaita watu Wake pamoja Kwake, katika umoja wa kweli na Yeye Mwenyewe, kwa sababu ni yule Roho Wake mmoja Mtakatifu. "Kwa Roho mmoja sote kibinafsi tumebatizwa katika Mwili mmoja, pamoja ni Mwili wa Yesu Kristo." Naye Yesu Kristo akiishi pamoja na Roho Wake katika mwili wetu, analitumikia Kanisa na kufanya mambo yale yale Yeye aliyoyafanya, kama i—ishara, kama bendera kwa ulimwengu, kwamba tuko katika siku za mwisho, tukijiweka tayari kwa ajili ya Unyakuo. Loo, nampenda, nanyi je?

210 Ninacho kitabu hapa bado, bali kamwe siwezi kukiendea tena, tunachelewa kupita kiasi. Huenda nikakichukua wakati mwingine.

211 Tuko mwisho. Umoja. Hivi wewe ni mmoja sana na Mungu? Hivyo ndivyo itakavyokubidi kuwa. Naam. Itatubidi kuwa mmoja na Yeye mpaka. . .Nia iliyokuwamo katika Kristo na

iwe ndani yenu. Ndipo Kristo, nia Yake Mwenyewe ndani yako italitambua kila Neno alililoliandika. Lilifanya hivyo katika mitume, wakiyatumia Maandiko kwa halali, ambayo ndiyo Kweli, mnaona, Roho Mtakatifu. Iwapo ni Kweli, basi Yeye atalishuhudia kwa kuleta ishara ile ile aliyompa Musa, ishara ile ile aliyompa Ibrahimu, ishara ile ile aliyofanya kwa Kristo, ishara ile ile aliyoifanya kwa Paulo. Tuko katika wakati wa mwisho. Yeye alisema hilo litakuwa. Tuko katika wakati wa mwisho. Kanisa, kwa jumla, linakusanyika pamoja katika muungano, mmoja hapa na mmoja pale, likiunganika.

212 Yeye alisema, "Wawili watakuwa kondeni, nitamchukua mmoja." Mmoja. Angalia, "Wawili kondeni," hiyo ni mchana, mavuno, "Nitamchukua mmoja na kumwacha mwingine. Wawili watakuwa kitandani," upande wa pili wa dunia, "nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja," katika kuja kwa Mwana wa Adamu. Nako kumekaribia sana, ni karibu sana.

213 Kamwe! Kamwe, Adamu! Adamu! Hawa, Adamu, hebu niwapazie sauti, msiusikilize uongo wa ibilisi tena. Dumuni na Neno la Mungu, Hilo ni BWANA ASEMA HIVI. Dumuni pamoja na Neno Lake. Kujitenga na Hilo ni kuuvunja ushirika wako na Mungu, umoja wa Mungu kwa Roho Mtakatifu. Ndipo kama ukisema unaye Roho Mtakatifu naye haafikiani na Neno, basi wewe si mmoja na Mungu.

214 Huu ndio umoja wa Mungu, wakati wewe. . .ro—roho uliye naye anapokubaliana na Neno hili, na kulidhihirisha Neno hili na kulifanya Neno hili nguvu kutenda vile vile lilivyotenda kule.

215 Hebu na tuliseme pamoja: "Umoja na Mungu ni kuwa na Roho wa Mungu ndani yako akikubaliana na Neno, Neno lote, Neno zima, na kulifanya Hilo lidhihirishwe katika nguvu."

216 Haya basi, huo ndio umoja na Mungu. Hapo nguvu hizo zinapotenda kazi ndani yangu, zinapotenda kazi ndani yako, sisi ni mmoja. Amina! Ndugu Kidd, wakati zile nguvu za Roho Mtakatifu ndani yangu zinapotenda kazi ndani yako, hakuna kuhitilafiana, Neno lipo hapo. Linatenda kazi. Amina. Linalifanya Hilo kile lilicho, Mungu aliyefanyika mwili ndani yako kwa Neno Lake. Neno lililofanyika nguvu miongoni mwenu, kila Neno!

217 Sasa, kumbukeni, ibilisi huchukua kiasi kikubwa cha Neno hilo, karibu sana asilimia tisini na tisa na tisini na tisa la Hilo. Tisini na tisa kwa mia na asilimia tisini na tisa ya hiyo mia, atalifanya Hilo kweli hasa, lakini basi ataruka atoke *hapa,* na hilo ndilo linalosababisha mauti papo hapo. Hilo huvunja huo mnyororo papo hapo katikati, nawe unaanguka.

218 Kila Neno! Yesu alisema nini? "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno!" Mtu hataishi kwa machache ya Maneno ya Mungu, si kwa tisini na tisa na asimia tisini na tisa ya Neno la

Mungu. Bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu, mtu ataishi kwa Hilo.

219 Shetani alimpandisha kule juu na kusema, “Imeandikwa!” Mnaona, kama vile tu alivyomwambia Hawa, “Imeandikwa! Imeandikwa!”

Yesu akasema, “Na pia imeandikwa . . . ”

220 Yeye alisema, “Imeandikwa, ‘Atakuagizia Malaika wake.’ Biblia ilisema hivyo!” Jamani, yeye ni mwanachuoni. “Imeandikwa, ‘Yeye atakuagizia Malaika Wake usije ukajikwaa mguu Wako katika jiwe, nao watakuchukua.’”

221 Akasema, “Pia imeandikwa, ‘Usimjaribu Bwana Mungu Wako.’”

222 Wakasema, “Tunayo Maandiko,” Matendo 19, “tulibatizwa na Yohana.”

223 Paulo alikuwa na kitu kingine, yeye alisema, “Huo haufanyi kazi tena.” Mnaona? “Yohana alibatiza tu . . . ” Yeye hakukosa kuliamini neno la Yohana. Alisema, “Nitawaambia yale Yohana aliyosema. Yohana alisema alibatiza kwa toba, sio kwa ondoleo la dhambi.” Dhabihu haikuwa imechinjwa, mnaona. Yeye alisema, “Alibatiza kwa toba, akisema mnapaswa kumwamini Yeye atakayekuja.” Basi waliposikia haya, walibatizwa katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Paulo akaweka mikono yake juu yao iliyojaa Neno sana, ndipo Roho Mtakatifu akashuka juu yao. Wakaanza kutabiri, kunena kwa lugha, kumtukuza Mungu, na ni wakati wa jinsi gani! Loo, jamani. Lilikuwa kanisa kubwa jinsi gani? Kumi na wawili. Naam. Loo, Mungu hafanyi kazi na idadi kubwa, Yeye hufanya kazi katika mioyo miaminifu. Hebu na tuwe na moyo wa namna hiyo. Mnampenda? Na tuombe.

224 Loo, mwenzangu mpendwa unayetangatanga, hivi umewaangalia binti za Moabu ama umewaona hao binti (ninazungumza juu ya makanisa) za Kaini? Jinsi yanavyopotoka na kwenda mbali na Neno! Hivi, rafiki yangu wa thamani, umeona katika siku hizi za mwisho kwamba mambo haya yametimia? Umekuwa ukiona hivi majuzi kuhusu jinsi Neno la Mungu linavyodhihirishwa? Jinsi ambavyo uamsho ambao wakati mmoja ulitokea sasa umetulia, hakuna mengi yaliyosalia? Ni kitu gani? Ni utulivu kabla ya dhoruba. Hukumu ziko tayari. Umekuwa ukiyang’amua mambo haya? Hivi umeyalinganisha Maandiko na Maandiko, Neno la Biblia na Neno la Biblia, thibitisho na thibitisho? Umelinganisha Neno la Yesu ambalo Yeye alisema ya kwamba ibilisi katika siku za mwisho . . . angefanana sana, kama kitu kilicho halisi, mpaka kama yamkini ingemdanganya kila mmoja ila Mteule, Yule Mteule. Wazieni tu, hilo fundisho la Kimaandiko litakuwa karibu sana! “Loo, tunamwamwini Roho Mtakatifu, Mungu abarikiwe milele! Tunaye Roho Mtakatifu, tunanena kwa lugha.” Kisha kugeuka

na kulikana Neno? Naam. Mnaona, itawadanganya walio Wateule kama yamkini.

225 Iwapo kuna mtu fulani humu ndani ambaye hayuko sawa na Mungu, ikiwa kuna mtu fulani hapa aliye mgonjwa ama anayeteseka. . .Kunazo leso na kadhalika zilizowekwa hapa, nitaziombea. Sijali unachohitaji. Kila ahadi katika hiki Kitabu ni yako. Ni yako.

226 Sasa, nimewaletea Neno, nikalileta kutoka Mwanzo hadi kwenye siku hizi tunazoishi, nikigusa tu mahali pengi na kuwaonyesha. Mamia mengi ya mahali ningeweza kugusia mbali na hayo, sina wakati. Lakini hakika, katika jambo hilo, mnaweza kuona ya kwamba upuuzi huu wa dhehebu uko nje. Ni dhana ya uongo ya ibilisi, akijaribu kumuundia mwanadamu dhehebu pamoja na umoja wa nia zao na mawazo yao wenyewe. Wakati, Roho Mtakatifu ndiye tunayeunganishwa kwa Mungu naye kama mmoja. Naye Roho Mtakatifu hukubaliana na Neno la Mungu. Mnaona, Biblia ilisema, Yesu alisema ya kwamba hata wangekiri, mnaona, "Wangewadanganya walio Wateule kama yamkini." Mnaona mahali tunaposimama?

227 Sasa litwae Neno hili la Mungu katika mkono huo wa imani. Unahitaji nini asubuhi ya leo? Una haja ya ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo? Kidimbwi kimefunguliwa. Unahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu? Yeye anajaribu kupenyeza njia Yake aingie ndani yako. Una haja ya uponyaji? Mbona, Roho Mtakatifu Mwenyewe, Neno ambalo limefanywa nguvu, yupo papa hapa sasa, nguvu zenyewe za utambuzi zikiangalia juu ya kusanyiko hili hapa sasa na kuiona ile Nuru ikizunguka kote kama mmeko. Hivi nimewahi kuwaambia jambo lolote lisilo kweli? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.]

228 Nimewahi, kama—kama yule nabii alivyowaambia Israeli kabla hawajampata mfalme wa kujibunia, alisema, "Je, nimewahi kuwaambia lolote. . .? Nimewahi kuzichukua pesa zenu? Nimewahi kushuka kuja na kuwaomba pesa na—na kuendesha huku na huku na kuishi katika majumba makubwa mno ya kifalme na kujenga vitu vikubwa mno na kuchukua pesa zenu kutoka kwenu? Hivi nimewahi kuwaomba hela moja?"

"La hasha."

229 Nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ila lile Mungu alilitimiza? Nimewahi kunena katika Jina Lake ila lile lililokuwa ni kweli? Nimewahi kuwaambia ono juu ya kusanyiko ila lile ambalo lilikuwa hasa huyo mtu aliamka, mgeni ama chochote anachoweza kuwa, ila lile alilosema "Hiyo ni kweli"? Je, nimewahi kuwaambia jambo lolote la uongo? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Basi hebu niwaambie sasa, BWANA ASEMA HIVI, mpokeeni Roho Mtakatifu, yule Roho atakayelichukua Neno la Mungu katika mikono hiyo ya imani,

asonge huko ng'ambo. Ufalme wote ni mali yenu. Ni wenu, enyi watoto.

230 Kwa nini mnakuja kutoka Georgia, kutoka kote nchini, kutoka Ohio, kutoka Kansas, kila mahali, kwa ajili ya mkutano mdogo? Nafikiri kanda imezimwa sasa, kwa hiyo, ninaweza kusema hili. Mnaona? Kwa nini mnakuja namna hii? Ni kitu gani kinachowafanya mfanye hivyo? Ni kitu gani? Ninawaona watu hapa kutoka Arkansas, kutoka umbali wa mamia ya maili.

231 Jana usiku, akitoka huko mbali kwenye Jiji la Kansas, maskini ndugu Mpolandi anayesimama kule nyuma, alikuja, akiongozwa, kasema, "Ndugu Branham, tangu niliposikia habari zako kwa mara ya kwanza huko nyuma katika Canada miaka mingi iliyopita, mambo ambayo umeyaona na kufanya, nimeyachunguza yote, mbele na nyuma, juu na chini," na kasema, "si hata moja ya hayo limewahi kukosea." Labda yeye ni Mpolandi Mkatoliki, naye huyu hapa anakuja, akizichukua kanda, akienda na kuzicheza, akikutana na upinzani. Wahudumu wanaopaswa kuwa pamoja nami na kutusaidia, bali wakikana Nguvu zake, wakiukana Ukweli wa Neno, huku wakidai kuwa na Roho Mtakatifu.

232 Sijajiita mwenyewe nabii. Mmefanya hivyo. Lakini, kama ndivyo ilivyo, basi Neno la Bwana linatoka wapi? Tunajuaje kama ni kweli ama si kweli isipokuwa kuwe na kitu cha kuliunga mkono? Hilo ni Neno la Mungu hapa, Neno lililoandikwa. Na basi kama Neno lililoandikwa limeungwa mkono, basi ni Mungu katika Neno hilo akilifanya hilo Neno kweli. Paulo alisema, "Nifuateni, kama ninavyomfuata Kristo."

233 Sasa, kama una haja na Mungu kwa ajili ya ugonjwa, kwa ajili ya wokovu, nini . . . ama kuondoa . . . Baadhi yenu wanawake msio na neema ya kutosha kuacha nywele zenu zikue, baadhi yenu wanaume msio na neema ya kutosha kuacha kuvuta sigara, baadhi yenu wahubiri msio na neema ya kutosha kuukubali ukweli wa ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, baadhi yenu watu mlio wagonjwa na mahututi, kwa nini msilichukue Neno hili asubuhi ya leo. Nitawaambia sasa, ni mwili miongoni mwetu! Lichukueni Neno hilo mkononi mwenu.

234 Hii hapa picha inayoning'inia ukutani, ya Malaika wa Bwana, Yule yule aliyewaongoza wana wa Israeli, Yule yule aliyekutana na Paulo, Yule yule aliyekuwa ndani ya Kristo. Na Roho Mtakatifu yeye yule yuko ndani yenu, ndani yenu, akiwaunganisha kuwa mmoja. Ni kitu gani kinachoivuta mioyo yetu pamoja kwa mamia ya maili? Hakuna kitu kama hicho nchini. Wanakuja kwenye Neno.

235 "Kuna chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wasioamini wanajitumbukiza chini ya hilo gharika, na kupoteza doa lao lote la hatia. Tangu kwa imani nilipokiona kijito hicho kilicholetwa na majeraha

Yako, upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo wangu, na utakuwa hata nitakapokufa."

236 Baba yetu wa Mbinguni, zilizowekwa hapa ni lundo la leso, glavu, huenda zikatumwa kwa barua. Sijui ni nani aliyeziweka hapa, labda ni Billy, labda ni watu hapa kwenye kusanyiko. Ninajisikia tu kufanya jambo hili sasa, Bwana. Hakuna kitu mikononi mwangu, hakuna kitu ndani yangu kama mwanadamu. Nisingeweza kuzitegemea akili zangu mwenyewe za kibinadamu. Sielewi ni kwa nini hili liko hivi, bali ninafuata yale uliyosema Wewe. "Walichukua kutoka kwa mwili wa Paulo, leso na nguo, na pepo wachafu wakawatoka watu." Haikuwa kwa sababu yeye alikuwa ni mtu mkuu, ilikuwa ni kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye katika Neno na nguvu. Wala hakushauriana na wale mitume, bali aliona walipokutana pamoja ya kwamba Injili ile ile, namna ile ile ya ubatizo, kila kitu kile kile walichokuwa wakifanya, kilikuwa ni kile kile hasa.

237 Sasa ninaomba, Bwana, kwa ajili ya watu hawa wa thamani wanaokuamini Wewe, ya kwamba Wewe utawaponya. Hao walio kwenye kusanyiko, waponye, Bwana. Jalia imani yao inyoshe tu mkono na kulishika Neno hilo sasa hivi, na kusema, "Kivimbe, maradhi, uovu, afadhali uondoke, ninakata kwa Upanga wa Mungu! Ninaamini! Imani yangu ina nguvu. Ninausukuma Upanga ndani kabisa. Ondoka njiani mwangu! Ninasimama kutoka kwenye kiti changu, nipate kuwa mzima." "Ninaweka mkono wangu juu ya baba yangu, juu ya dada yangu, mtoto wangu, juu ya jirani yangu. Ninaamini. Neno Lako ni Kweli. Niko katika umoja na Wewe. Kazi ulizosema Wewe kwamba Wewe ulizifanya, tungezifanya pia. Bwana Mungu, ninaamini kila Neno. Nami ninakuja mbele, ninakuja mbele kuudai, kuuchukua asubuhi ya leo."

238 Ee Mungu, jinsi ningewazia wakati kanisa lilipokuwa likisonga, wakati Musa alipohofia kidogo huko chini baharini, akaanza kumlilia Bwana. Ndipo Bwana akasema, "Mbona unanililia Mimi? Ni kwa nini unanililia Mimi? Nena na usonge mbele! Hivi sijakuagiza kwenye hii kazi? Nena!" Kunena nini? Neno la Mungu. "Liko ndani yako. Nena na usonge mbele. Usinililie Mimi. Endeleeni mbele."

239 Na, Bwana Mungu, leo naja katika Jina la Bwana Yesu. Naja nikiushika Upanga huu wa imani, nikidai umoja wa Mungu na mwanadamu kwa Roho Mtakatifu, kupitia kwa rehema na dhabihu ya Yesu Kristo Mwana Wake. Ninamwasi kila ibilisi aliyemfunga mtu yeyote katika njia yoyote katika jengo hili, kama ni mvulana ama msichana, mwanamume ama mwanamke. Ninayaasi kila maradhi. Ninaasi kila shaka. Ninauasi kila woga. Ninaasi kila kitu ambacho si cha kitauwa, liache kusanyiko hili katika Jina la Yesu Kristo! Toka kwenye kusanyiko hili, tupate kuwa mmoja na Mungu na tunaweza kumtumikia Mungu pasipo maradhi wala woga. Jalia nguvu zilizotufanya mmoja na

Mungu . . . Ibilisi huyo anawezaje kunguruma mwenyewe karibu na waliopakwa mafuta? Ibilisi anawezaje kusimama huko nje na kunguruma kama Goliathi? Wakati Daudi alipoingia kambini, na kusema, "Mnataka kuniambia mtamwacha Mfilisti huyo asiyetahiriwa asimame pale na kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai?"

240 Ee Mungu, wafanye wanaume na wanawake wasimame katika nguvu za Roho. Kumwacha ibilisi huyo asiyeongoka, msumbufu ambaye ameumiza jamii ya binadamu kote katika wakati, asimame hapa na kulitukana kanisa la Mungu aliye hai? Ewe Shetani, toka, na uondoke, katika Jina la Yesu Kristo!

241 Sasa, ninyi mlio na nguvu za kutosha kuutumia Upanga, sasa kwa kuwa una ufahamu wa kutosha katika Neno la Mungu kulidai Hilo kuwa mali yako binafsi, ni nani anaweza kulitwaa Neno la Mungu sasa mkononi mwako, ulishike Hilo katika mkono wa imani, na kusema, "Ninauchukua upande wangu pamoja na Bwana. Nitakuwa umoja na Mungu wangu, tangu sasa na kuendelea. Nitautumia Upanga huu wa Roho katika Neno hili, nami nitamkata ibilisi kwa kila ahadi ambayo Mungu aliniahidi mimi."

242 Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote, ninakuomba basi kwa unyofu kwa moyo wangu wote, katika Jina la Yesu Kristo, usimame kwa miguu yako na kulikubali. Je, unamaanisha hilo? Hivi wewe ni mwaminifu? Neno liko mkononi mwako? Mkono wako ndio imani yako? Mwinulie Mungu mkono wako wa kawaida, useme, "Mungu, kwa huu, kwa mkono wangu ulioinuliwa ninayatoa maisha yangu yote. Ninaitoa nafsi yangu, ninayatoa mawazo yangu, ninatoa kila kitu kwa Neno la Mungu. Jalia Roho Mtakatifu aichukue imani yangu sasa na kunipa hicho kitu. Akatilie mbali kila shaka kutoka kwangu. Na, kwa imani, ninaipokea ahadi ninayoomba, wakati huu."

243 Kama mnaliamini, semeni, "Amina," sasa. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Semeni, "Amina," tena. ["Amina."] Amina, amina, amina! Basi, kama unamaanisha hilo kwa moyo wako wote, katika Jina la Yesu Kristo, ninakuahidi ulichoomba. Amina. Wewe amini hilo kwa moyo wako wote. Mungu awabariki.

Ndugu Neville.

*UMOJA* SWA62-0211
(Oneness)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 11 Februari, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org